


# Huduma ya Mauti

Adrian Ebens

# Huduma ya Mauti

Toleo la Tatu

Ari kwa rafiki zangu wote
katika mtandao wa Facebook wa *Father of Love*.

Shukurani kwa kunihimiza na kuniombea na
kunisihi niendelee kusoma mstari baada ya mstari na kanuni juu ya kanuni
kudhihirisha kwamba kweli Baba yetu ni Upendo.

Kimechapishwa na

MARANATHA
MEDIA

maranathamedia.com

Kiliandaliwa katika Mwezi Mpya wa Disemba 1, 2016
kiliboreshwa Machi 4, 2018

# Yaliyomo


Huduma ya Mauti ........ 4
Dhambi Iletayo Mauti ........ 6
Dhambi Huficha Uso wa Baba ........ 7
Kifo cha Kristo Kilidhihirisha Nini? ........ 8
Kristo Anachoma Viza ........ 10
Kristo Hutuweka Huru Kutoka Kwa Hofu ya Mauti ........ 11
Msalaba Huelezea Hukumu Yote ya Mungu ........ 13
Tunahukumiwa Kwa Jinsi Tunavyo hukumu ........ 14
Muhtasari wa Awali ........ 15
Ibada ya Sanamu ya Ndama wa Dhahabu na Adhabu yake ........ 16
Unasoma Jinsi Gani? ........ 18
Kupima Kwa Uzima na Mauti ya Kristo ........ 19
Yesu anadhihirisha Jina/Tabia ya Baba ........ 20
Yesu Kama Hakimu ........ 22
Abrahamu Anaagizwa Kumuua Mwanawe ........ 29
Kuadhibu Dhambi kwa Dhambi ........ 31
Eliya na Matumizi ya Upanga ........ 33
Kasi ya Musa ........ 40
Unabii wa Yakobo kuhusu Lawi ........ 41
Kutolewa Kama Fidia ........ 45

# Huduma ya Mauti

> 2 Kor 3:7 Basi ikiwa ile huduma iliyoleta mauti, ile iliyoandikwa kwa herufi juu ya jiwe ilikuja kwa utukufu hata ikawa Waisraeli hawawezi kuutazama uso wa Mose kwa sababu ya ule utukufu wake, ingawa ulikuwa ni wa kufifia:

Huduma hii iliyoleta mauti ni nini? Inatwambia kwamba imeandikwa kwa herufi juu ya jiwe. Ni nini kilichoandikwa kwa herufi juu ya jiwe?

> Kut 31:18 Hapo Bwana alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika mlima wa Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu.

Hizi ni Amri Kumi. Hivyo Bibilia inatwambia kwamba Amri Kumi ni huduma iliyoleta mauti. Basi tunafahamu aje marejeleo haya ya sheria?

> Zaburi 1:2-3 Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. (3) Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.

> Zaburi 119:96-98 Nimeona ukamilifu wote kuwa na mwisho, Bali agizo lako ni pana mno. (97) Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa. (98) Maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu, Kwa maana ninayo sikuzote.

> Methali 13:14 Sheria ya mwenye akili ni chemchemi ya uzima, Ili kuepukana na tanzi za mauti.

> Yakobo 2:12 Hivyo semeni na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru.

Ni jinsi gani Sheria iletao mauti inaweza kuwa kwa wakati huo huo chemchemi ya uzima na uhuru? Inategemea mahali ambapo unasimama na miwani ambayo umevalia unapoitazama Sheria. Paulo anaelezea hili kwa makini na kwa upana katika mafungu yafuatayo:

> Rum 7:5-14 Kwa maana tulipokuwa tunatawaliwa na asili ya dhambi, tamaa za dhambi zilizochochewa na sheria zilikuwa zikitenda kazi katika miili yetu, hivyo tulizaa matunda ya mauti. (6) Lakini sasa, **kwa kufia kile kilichokuwa kimetufunga kwanza, tumewekwa huru kutoka katika sheria**

**ili tutumike katika njia mpya ya Roho, wala si katika njia ya zamani ya sheria iliyoandikwa. Sheria Na Dhambi** (7) Tuseme nini basi? Kwamba sheria ni dhambi? La, hasha! Lakini, ni kwa sababu ya sheria nisingekuwa nimeijua dhambi. Nisingekuwa nimejua kutamani ni nini kama sheria haikusema, "Usitamani." (8) Lakini dhambi kwa kupata nafasi katika amri, hii ikazaa ndani yangu kila aina ya tamaa. **Kwa maana pasipo sheria, dhambi imekufa.** (9) **Wakati fulani nilikuwa hai pasipo sheria, lakini amri ilipokuja, dhambi ikawa hai, nami nikafa.** (10) **Nikaona kwamba ile amri iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta mauti.** (11) **Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri, ikaniua.** (12) Hivyo basi, sheria yenyewe ni takatifu na amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema. (13) **Je, kile kilicho chema basi kilikuwa mauti kwangu? La, hasha! Lakini ili dhambi itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta mauti ndani yangu kupitia kile kilichokuwa chema, ili kwa njia ya amri dhambi izidi kuwa mbaya kupita kiasi. Mgongano Wa Ndani** (14) Kwa maana tunajua kwamba sheria ni ya kiroho, lakini mimi ni wa kimwili nikiwa nimeuzwa kwenye utumwa wa dhambi.

Wakati ambao hatuna ufahamu wa Sheria, hatuna ufahamu wa dhambi; uasi hauonekani.

Rum 4:15 kwa sababu sheria huleta ghadhabu. Mahali ambapo hakuna sheria hakuna makosa.

Sheria inapoingia, dhambi huhuika na tunakuwa chini ya hukumu ya Sheria.

Rum 5:20-21 Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. (21) Ili kwamba kama vile dhambi ilivyotawala kwa njia ya mauti, vivyo hivyo neema iweze kutawala kwa njia ya kuhesabiwa haki hata uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu.

Katika Warumi 7:9 Paulo anasema kwamba amri ilipokuja dhambi ilihuika nami nikafa. Paulo alikufa aje na bado akawa hai?

Rum 6:3-4 Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti Yake? (4) Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti, ili kama vile Kristo alivyofufuka kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia tupate kuenenda katika upya wa uzima.

# Dhambi Iletayo Mauti

Paulo alikufa na kisha akafufuka katika Kristo. Kwa wale ambao wanaamini, tayari wamepita kutoka kwa mauti hadi kwa uzima. Tunaendelea na mchakato huu wa mauti:

> Warumi 7:11 Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri, ikaniua.
>
> Warumi 7:13 Je, kile kilicho chema basi kilikuwa mauti kwangu? La, hasha! Lakini ili dhambi itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta mauti ndani yangu kupitia kile kilichokuwa chema, ili kwa njia ya amri dhambi izidi kuwa mbaya kupita kiasi.

Sheria ilileta je mauti ndani ya Paulo? Sheria ilifanya dhambi ionekane kuwa kuu zaidi. Na hili linafanikisha nini?

> Warumi 3:19 Basi tunajua ya kwamba cho chote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu.

Paulo alihukumiwa na maisha yake ya dhambi. Alijihisi mwenye hatia. Aliona kwamba alistahili kufa. Nini ambacho kilimfanya kuona kwamba alistahili kufa?

> Rum 7:13 ...Lakini ili dhambi itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta mauti ndani yangu kupitia kile kilichokuwa chema, ili kwa njia ya amri dhambi izidi kuwa mbaya kupita kiasi.

Ni dhambi ndio ilileta mauti ndani yake *kwa njia ya Amri*. Hili lina maana gani? Maajabu yote ya mchakato wa ukombozi yanapatikana katika msalaba wa Kristo. Nini ambacho kilileta mauti ndani ya Kristo?

> 2 Kor 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.
>
> Mwana wa Mungu alipoinama katika mkao wa maombi katika Bustani ya Gethsemani, uchungu wa Roho yake ulisukuma jasho kama matone makubwa ya damu. Hapa ndipo kitisho kikuu cha giza kilimzunguka. Dhambi za ulimwengu zilikuwa juu yake. **Alikuwa akiteseka kwa niaba ya mwanadamu kama mdhambi wa sheria ya Baba yake.** 2T 203

Dhambi ilikuwa ikileta mauti ndani ya Kristo kwa njia ya amri ya Baba. Kitisho ambacho kiliingia kwa Kristo kilikuwa utambuzi wa jinsi dhambi ilivyo ya kutisha na yenye uharibifu. Nuru ya kitisho hiki inatoka wapi? Inatoka kwa sheria. Hili linafanya sheria kuwa wakala mtendaji wa mauti?

> Rum 7; 11,12 **Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri, ikaniua.** (12) Hivyo basi, sheria yenyewe ni takatifu na amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema.

Dhambi hutenda uuaji wa nafsi, ingawa hufanya hivyo kwa kudanganya nafsi kupitia kwa amri. Katika hali ya Paulo imani yake katika Kristo ilimruhusu kuepuka kifo halisi wakati huo lakini katika hali ya Kristo kifo halisi hakikuondolewa. Mbona hivi? Ni kwa sababu tu *alikufa kama ambaye hangeuona uso wa Baba yake*.

> Kristo hakujitoa kwa adui wenye kutesa, hata katika maumivu makali. Majeshi ya malaika waovu yalimzunguka kote; ila malaika watakatifu walionywa wasivunje vyeo vyao, na kuingia kwenye mgogoro kwa vurugu, kutusi adui, wala hawakuruhusiwa kuhudumia roho iliyoumizwa ya mtesekaji Mtakatifu. Ni katika saa hii ya giza ya kutisha, **uso wa Baba yake ulifichwa, majeshi ya malaika waovu yakimzunguka, dhambi za ulimwengu zikiwa juu yake, kwamba kutoka kwa midomo yake iliyosafura kulitoka maneno, "Mungu wagu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"—** Bible Echo and Signs of the Times, Januari 1, 1887.

## Dhambi Huficha Uso wa Baba

Nini kiliuficha uso wa Baba? Dhambi. Dhambi huficha uso wa Baba kwa njia gani? Humuonyesha kama ambaye hayuko tayari kusamehe. Humuonyesha kama ambaye huhitaji kifo cha kila mdhambi. Dhana hii ilitoka wapi?

> Katika kuanzishwa kwa pambano kuu, Shetani alikuwa ametangaza kwamba sheria ya Mungu haiwezi kutunzwa, kwamba haki haiendani na rehema, na kwamba, sheria ikivunjwa, **haiwezekani mdhambi kusamehewa. Kila dhambi lazima ipokee adhabu yake, shetani alisisitiza;** na kama ataondoa adhabu ya dhambi, hatakuwa Mungu wa kweli na haki. DA 761

> Nguvu ya kuhukumu ya Shetani ingemuongoza kuanzisha nadharia ya haki isiyoendana na rehema. Hudai kusimamia kama sauti na nguvu ya

Mungu, anadai kuwa maamuzi yake ni ya kweli, safi na hayana dosari. Kwa hivyo anachukua nafasi yake kwenye kiti cha hukumu na kutangaza kuwa mashauri yake hayawezi anguka. **Hapa ndipo rehema yake bila huruma inaingilia, haki ghushi, adui na mawazo ya Mungu.** CTr 11.4

Shetani aliketi kwenye kiti cha hukumu na kuanzisha nadharia ya haki ambayo ilimaanisha kwamba kila dhambi lazima iadhibiwe bila huruma.

Wengi walielekea kujihadhari na mashauri haya, kutubu hisia za kukengeuka kwao, na kutafuta kupokelewa tena kwa fadhila ya Baba na Mwanawe. Lakini Lusifa alikuwa na uongo mwingine tayari. Muasi mkuu sasa alitangaza kuwa malaika ambao walikuwa wameungana naye walikuwa wameenda mbali sana kiasi ya kwamba hawangeweza kurudi; kwamba alikuwa anajua sheria takatifu, **na alijua kwamba Mungu hawezi samehe.** PP 40

Pendekezo hili lilimaanisha kwamba wakati ambao haki inatekelezwa rehema inaondolewa. Bila shaka dhana hii ya haki humaanisha kwamba rehema haiko kabisa kwa sababu kila dhambi lazima iadhibiwe. Hakuna huruma. Popote ambapo haki hutolewa bila huruma, ni kauli ya mfumo wa shetani wa haki bila huruma ambao alianzisha kuchafua tabia ya Mungu na kuzuia malaika wasirejee kwake. Mfumo huu wa uongo ulikuwa adui wa mawazo ya Mungu.

## Kifo cha Kristo Kilidhihirisha Nini?

Upendo wa Mungu umedhihirishwa katika haki yake sio zaidi kuliko katika rehema yake. Haki ni msingi wa enzi yake, na tunda la upendo wake. Limekuwa kusudi la Shetani kuondoa fadhili kutoka kwa ukweli na haki. Alijaribu kuthibitisha kwamba haki ya sheria ya Mungu ni adui kwa amani. Lakini Kristo anaonyesha kwamba katika Mpango wa Mungu zimeunganishwa pamoja na haziwezi tenganishwa; moja haiwezi kuwepo bila nyingine. "Fadhili na kweli zimekutana, Haki na amani zimehusiana." Zaburi 85:10 **kwa maisha yake na kifo chake, Kristo alithibitisha kwamba haki ya Mungu haikuharibu fadhili zake, ila kwamba dhambi inaweza samehewa, na kwamba sheria ni ya haki, na inaweza ikatunzwa kikamilifu. Mashtaka ya Shetani yalikanushwa. Mungu alikuwa amempa mwanadamu ushahidi thabiti wa upendo wake.** {DA 762.3,4}

Ni jinsi gani Kristo alidhihirisha upendo wa Mungu na chuki ya Shetani kwa wakati mmoja? Ni jinsi gani Msalaba ni ufunuo wa upendo usiokuwa na mwisho wakati ambao unaonyesha joka mtini?

> Hisia za kuondolewa kwa upendo wa Baba yake zilisonga kutoka kwa nafsi yake yenye uchungu maneno haya ya kuomboleza: "Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa." 2 T 206
>
> Dhambi za ulimwengu uliopotea zilikuwa juu yake na kumlemea. Ni hisia ya Baba yake kukunja uso, kwa athari za dhambi, zilizofarakanisha moyo wake na uchungu wa kuchoma jinsi hiyo na kulazimisha matone ya damu kutoka kwa paji la uso wake, ambayo, yakitiririka kwa mashavu yake yaliyosafura, yalianguka ardhini, yakilowesha nchi. 2T 204.1
>
> Kristo alihisi jinsi wadhambi watahisi wakati bakuli za ghadhabu ya Mungu zitamwagwa juu yao. Kukatizwa tamaa kweusi, kama subahiya ya kifo, kutaizunguka mioyo yao yenye hatia, na kisha watatambua kikamilifu kiwango cha uovu wa dhambi. 2T 210
>
> Kristo alihisi uchungu ambao mdhambi atahisi wakati ambao fadhili haiwezi tetea jamii yenye hatia. DA 753

Mbona Kristo akafa msalabani? Alikufa kama vile mdhambi angekufa. Mbona mdhambi afe? Sheria humtia hatiani kwa dhambi, hukataa kuamini kwamba Mungu anaweza msamehe na kwa hivyo hufa. Yesu na Baba walionyesha mfumo wa haki wa Shetani kwa Ulimwengu. Kristo alibeba hali yetu ya dhambi juu yake; alihisi hukumu ya kutisha ya dhambi kwamba wakati wote Baba yuko tayari kusamehe kwa huruma zake lakini kwa Kristo hangenyoosha mkono wake na kuuchukua mkono wa upendo wa Baba yake kwa sababu mdhambi hawezi fanya hilo na kwa hivyo angekufa jinsi ambavyo wadhambi hufa – bila kuamini kwamba Mungu anaweza wasamehe.

> Mwanz 4:13 Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki.

Wakati kristo alichukua hali yetu ya dhambi juu yake, ilificha uso wa Baba – dhambi ilificha uso wa Baba, sio Baba alificha uso wake. Tofauti ni muhimu sana. Alikuwa tayari kurehemu lakini dhambi iliufunika uso wake ili kwamba Kristo alilia:

> Mat 27:46 Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia, “Eloi, Eloi lama sabakthani?” Maana yake, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?”

Hiki ni kilio cha mtu ambaye amebeba dhambi zetu zote. Mbona alinena maneno haya? Alinena maneno haya kwa sababu alifanywa dhambi kwa ajili yetu. Dhambi ilichukua fursa kwa amri na ikamuua Kristo.

## Kristo Anachoma Viza

Kristo alipokuwa karibu kukata roho, yote ambayo Kristo alijua kumhusu Baba yalichoma viza kwa dakika na akasema:

> Luka 23:46 Yesu akapaza sauti Yake akasema, “Baba, mikononi mwako naikabidhi roho Yangu.” Baada ya kusema haya, akakata roho.

Alihisi kuhukumiwa na kulemewa na katika dakika ya mwisho aliamua kuamini kuwa Baba angempokea hata ingawa ilionekana kuwa haingewezekana.

> Shetani na majaribu yake ya kutisha alipiga moyo wa Yesu. Mkombozi hangeona kupitia kwa mianya ya kaburi. Tumaini halikuwasilisha kwake kutoka kwake kwenye kaburi akiwa mshindi, au kumwambia kukubaliwa kwa kafara na Baba. Alihofu kwamba dhambi ilikuwa mbaya kwa Mungu kwamba utengano wao ungekuwa wa milele. Kristo alihisi uchungu ambao mdhambi atahisi wakati ambao fadhili haiwezi tetea jamii yenye hatia. Ni hisia ya dhambi, ikileta ghadhabu ya Mungu juu yake kama kibadala cha mwanadamu, ilifanya kikombe ambacho alinywea kuwa kichungu, na kuvunja moyo wa Mwana wa Mungu. {DA 753.2}

> Hakuna jicho lingepenyeza kwenye giza ambalo liliuzunguka msalaba, hakuna yeyote angepenya giza kuu ambalo liliuzunguka moyo wa kuteseka wa Kristo. Umeme wenye hasira ulionekana kuwa pigo kwake aliponinginia kwenye msalaba. Kisha “Yesu akapaza sauti akalia, “Eloi, Eloi lama sabakthani?” Maana yake, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” giza la nje lilipotulia kwa Mkombozi, sauti nyingi zilisema: kisasi cha mbinguni ki juu yake. Komeo za ghadhabu ya Mungu ni pigo kwake, kwa sababu alidai kuwa Mwana wa Mungu. Wengi ambao walimwamini walisikia kilio chake cha kukata tamaa. Tumaini liliwaondoka. Kama Mungu alikuwa amemwacha Yesu, wafuasi wake wangeamini nini? DA 754

> Ghafla giza liliinuliwa kutoka kwa msalaba, na katika toni kama ya tarumbeta, yenye kusikika vizuri, ambayo ilionekena kusikika kwa maumbile yote, "Yesu akapaza sauti Yake akasema, "Baba, mikononi mwako naikabidhi roho Yangu." Mwanga uliuzunguka msalaba, na uso wa Mkombozi uling'a kwa utukufu kama jua. Kisha akainamisha kichwa chake kifuani mwake, na akafa. {DA 756.2}

Kilio hicho ambacho kilichoma viza na kumshika Baba ni ukombozi wetu. Mwanga ambao uliuzunguka msalaba ni ushahidi wa kukubalika na Baba kutoka kwa shimo la jehanamu. Ushindi wake ni wetu. Kifo chake kilidhihirisha mfumo wa haki wa shetani na imani yake ikichoma wingu la dhambi zetu ilifanikisha ukombozi wetu. Ulifanikishwa kwa njia gani? Aliamini kwamba bado Baba angempokea ingawa kila sehemu ya nafsi yake ilisema kuwa haiwezekani.

Ni imani sawa iliyodhihirishwa katika Ibrahimu wakati ambao alikuwa amewekwa chini kwa mateso ya kutisha katika wazo la kumuua mwanawe. Alipoingia kwenye giza aliamua kuamini kwamba Mungu angefanya litendeke kwa wema na kuitekeleza ahadi yake.

Ni sawa na ile ya mwanamke wa Kanani ambaye alikabiliana na kunyamazishwa kwa Yesu na kile ambacho kilionekana kuwa kauli kwamba alikuwa mbwa. Dhambi ilificha uso wake kutoka kwake. Dhambi gani? Ilikuwa chuki ya kikabila ya wayahudi na Wakanani. Dhambi hii ilificha uso wa Yesu kutoka kwa mwanamke huyo, ingawa roho wa Kristo ndani yake, ilichoma kufichwa kwa uso, na alinena maneno yenye utukufu:

> Matt 15:26-27 Yesu akajibu, "Si haki kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." (27) Yule mwanamke akajibu, "Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza za bwana zao."

## Kristo Hutuweka Huru Kutoka Kwa Hofu ya Mauti

Adamu alipotenda dhambi aliingizwa kwa mfumo wa Shetani ambao hauna huruma kwamba kila adhabu lazima itekelezwe na kama Mungu alivyosema kwamba kula tunda kulimaanisha kifo, Adamu alipokea dhana kwamba hakika Mungu atamtia katika mauti. Hili lilimweka Adamu kwenye kiziba cha utumwa.

> Ebr 2:15 na kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti.

Mwana wa Mungu alikuja kuvunja nguvu za mauti kwa kupenyeza kupitia kwa viza vya haki ya Shetani isiyokuwa na huruma. Msalabani alijishusha hadi ambapo mwanadamu alisimama. Mwanadamu alisimama mahali pa kuamini kwamba dhambi zetu ni kuu kiasi cha kutosamehewa. Katika hali hii hii Mwana wa Mungu aliiweka Roho yake mikononi mwa Baba. Kwa kufanya hivi aliufunga ufalme wa Shetani. Yeshua Mkombozi wetu alifunua uongo kwamba Baba hawezi tupokea. Na kwa hivyo tunasoma:

> Ebr 2:14 Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao, ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani, Shetani;
>
> Mwana wa Mungu asiyekuwa na mawaa aliniginia msalabani, mwili wake ulivimba kwa kupigwa; ile mikono ambayo mara nyingi iliwafikia wengi kwa mibaraka, iligongelewa misumari kwenye mbao, miguu ile ambayo ilihudumu kwa upendo bila kuchoka, ikishikanishwa kwenye mti; hicho kichwa cha kifalme kikichomwa na taji la miiba; midomo hiyo yenye mtetemeko—matone ya damu ambayo yalitiririka kutoka kichwani mwake, mikononi mwake, miguu yake, uchungu ambao ulipiga sura yake. Na uchungu usioelezeka ambao ulijaza nafsi yake kwa kufichika kwa uso wa Baba yake—yananena kwa kila mwana wa adamu, yakitangaza, **ni kwa ajili yako Mwana wa Mungu alikubali kubeba mzgo huu wa hatia; kwa sababu yako anaharibu utawala wa mauti, na kufungua milango ya Paradiso.** DA 755

Kwa kuchukua hali yetu, Kristo alijiweka mahali ambapo mwanadamu alisimama katika kuamini kwamba Mungu anahaki bila huruma na kutoka mahali hapa alijipeana kwa Baba yake akiamini kwamba atakubalika licha ya hisia zake zote.

Bwana Yesu Mpendwa ni jinsi gani ulivyomwema. Wewe ni njia, ukweli na uzima. Umemfunua jika msalabani na kudhihirisha mfumo wake wa haki bila huruma na kudhihirisha kwamba Baba yuko tayari kutupokea.

## Msalaba Huelezea Hukumu Yote ya Mungu

Mara tutakapouelewa msalaba basi tunaweza elewa visa vingi ambavyo vinaonekana kuwa vikali na vya kutisha.

> Ajabu ya msalaba huelezea maajabu mengine yote. Katika nuru ambayo hutiririka kutoka Kalvari sifa za Mungu ambazo zilikuwa zimetujaza na hofu na uoga zinaonekana kupendeza na kuvutia. Rehema, huruma, na upendo zinaonekana kuchanganyika na utukufu, haki na uwezo. Tunapotazama ukuu wa enzi yake, juu na kuinuka zaidi, tunaona tabia yake katika dhihirisho la neema yake, na kufahamu, kuliko awali, umuhimu wa jina hilo la kupendeza, "Baba Yetu." {GC 652.1}

Kisa cha msalaba hutufundisha kwamba ni dhambi ndiyo ilileta mauti kupitia kwa sheria. Kwa hili tunamaanisha kwamba mdhambi haamini kwamba Mungu husamehe dhambi. Yeshua alivunja utawala wa kifo kwa kusimama katika kikoa hicho na kuchagua kuamini Baba alimkubali. Hili lilifunga kabisa uongo kuhusu tabia ya Mungu kama hakimu ambaye hana huruma. Ilidhihirisha kwamba dhambi ilikuwa mwangamizi; dhambi ilisababisha uso wa Baba kufichwa; dhambi ilizuia mkono kunyooshwa na kuamini msamaha. Dhambi ndiyo iliwasukuma Mafarisayo kumhukumu Yesu; dhambi ndiyo ilimfanya Pilato kushirikiana na viongozi wa Wayahudi; dhambi ndiyo ilimfanya Yuda amsaliti; dhambi ndiyo ilimsulubisha Yesu msalabani.

Mbona basi uongo huu wa Baba yetu kuwa hakimu asiye kuwa na huruma unadumu? Ni kwa sababu Shetani huugeuza msalaba kuwa tendo la Mungu.

> Isa 53:3-4 Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. (4) Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa.

Msalaba hudhihirisha kwetu upendo wa ajabu wa Baba lakini dhambi kupitia kwa sheria hutudanganya na kutufanya kuamini kwamba Mungu alihitaji kifo ili kuridhisha hasira yake dhidi ya dhambi. Sio tu alihitaji hilo bali pia kwamba Mungu mwenyewe alimuua Mwanawe. Isaya 53 inatwambia kwamba tunauangalia msalaba kwa njia hii. Tunaposoma hukumu za Mungu katika Agano la Kale kama mdhambi akiangamizwa na Mungu mwenyewe

tunadhihirisha ufahamu wetu wa msalaba. Tunapowaangalia wale ambao walikufa kama walipigwa na Mungu na kuteswa basi tunakubaliana na Shetani kwamba Mungu ni mwenye hukumu isiyokuwa na huruma kwa kutumia nguvu isioepuka kifo kwa wale ambao humkosea. Kila tukio katika Bibilia ambapo watu hufa kupitia kwa hukumu tunahimizwa kuutazama msalaba. Mbona hivi?

> Wachache huwaza kuhusu mateso ambayo dhambi imemletea Muumbaji wetu. Mbingu yote iliteseka katika uchungu wa Kristo; lakini kuteska hukwo hakukuanza wa kukamilika na kujihidhirisha kwake katika ubinadamu. **Msalaba ni ufunuo kwa hisia zetu za giza za uchungu ambao, tangia kuanzishwa kwake, dhambi imeleta kwa moyo wa Mungu.** Kila kuondoka kwa nuru, kila tendo la ukatili, kila kushindwa kwa mwanadamu kufikia matakwa, huleta huzuni kwake. **Majanga yalipokuja kwa Israeli ambayo yalikuwa tokea thabiti la utangano na Mungu,—kutawaliwa na adui zao, ukatili, na kifo,—inasemekana kwamba "Roho yake ilihuzunika kwa sababu ya msiba wa Israeli."** "**Katika mateso yao yote yeye aliteswa: ... akawainua, akawachukua siku zote za kale.**" Waamuzi 10:16; Isaya 63:9. – Ed 263.1

Baba yetu na Bwana Yesu hawapendi hata mmoja kufa. Huwasababishia uchungu mwingi kwa mdhambi aangamiae.

> 2 Pet 3:9 Bwana hakawii kuitimiza ahadi Yake kama watu wengine wanavyodhani kukawia, bali Yeye anawavumilia, maana hataki mtu ye yote aangamie, bali kila mmoja afikilie toba.

## Tunahukumiwa Kwa Jinsi Tunavyo hukumu

Mbona wote hawafikiri toba? Ni kwa sababu hawaamini kwamba Mungu anaweza wasamehe. Gundua kwamba hukumu yetu ya wale ambao waliadhibiwa katika Agano la Kale na kifo cha mwisho cha waovu itakuwa mfumo wa hukumu ambao tutautumia juu yetu.

> Matt 7:2 Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea.

Katika visa vyote vya Bibilia ambapo hukumu inawaangukia watu, tukisoma visa hivi kama Mungu kamwe hatoi msamaha kwao bali kuuondoa mkono

wake wa rehema ili kuwaangamiza, basi hivi ndivyo tutakavyojihukumu wakati ambao hatia ya dhambi hutujia kupitia kwa Sheria.

Tafadhali usipitwe na hoja hii. Mungu hututumia hatia ya dhambi ili kutuokoa. Kama tunaamini kwamba Mungu hufikia pahali ambapo huondoa karama hiyo basi hatuwezi vumilia kipindi cha mateso ya Yakobo. Dhambi zetu zitatuvunja zinapodhihirishwa kwetu. Tutateswa na maisha yetu ya dhambi kupitia kwa sheria lakini wale ambao wamechagua kuamini kwamba mkono wa rehema wakati wote unapitishwa kwao kamwe hawajachelewa kupenyeza giza la hukumu yetu na kuokolewa. Naomba uweze kushika umuhimu wa maneno haya. Yatathibitisha wokovu wako au laana kutegemea jinsi unavyochagua kuzipokea.

Bibilia inatwambia:

> Zab 86:5 Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao.

> Zab 100:5 Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele; Na uaminifu wake vizazi na vizazi.

Rehema ya Mungu ni ya milele. Haiishi kwa wakati wowote. Huisha tu kwa wale ambao hawaiamini.

> Zab 86:13 Maana fadhili zako kwangu ni nyingi sana; Umeiopoa nafsi yangu na kuzimu.

Kuzimu ni nini? Ni mahali ambapo unahisi kwamba hakika hauwezi samehewa. Mungu anaweza kuopoa kutoka kwa hili ukiamini.

## Muhtasari wa Awali

Sasa wacha tufupishe yale ambayo tumeangalia hadi sasa:

1. Sheria huleta mauti kwa mwanadamu aliye katika dhambi na uzima kwa mwanadamu aliye katika haki. Rum 7:5-13
2. Mwanadamu wa mwili hukubali uongo wa Shetani kwamba uasi lazima uadhibiwe kwa mauti na kwamba haina haja kuomba msamaha. Gal 3:10

3. Sheria hututia hukumuni kwa dhambi ili kuturehemu, lakini mwanadamu wa mwili huelewa hukumu kama utangulizi wa kifo cha hakika. Yohana 16:8; Mwanz 4:13 (kiasi)
4. Rehema za Mungu ni za milele. Zab 100:5. Muovu hujihukumu kwa mauti na maangamizi. Rum 1:32; Mwanz 4:13 (kiasi); Hes 14:28
5. Kristo hudhihirisha uongo wa Shetani kupitia kwa kifo chake msalabani. Kupitia kwa kifo aliangamiza huyo mwenye nguvu za mauti. Ebr 2:14
6. Kristo alichukua dhambi zetu juu yake na akafa jinsi ambavyo mdhambi hufa ili kudhihirisha kwamba dhambi husababisha kifo. 2 Kor 5:21
7. Katika kina cha ndani cha kuzimu kwa mateso makubwa Kristo alijiweka mikononi mwa Baba na kwa hivyo kufunga utawala wa mauti. Matt 27:46; Luka 23:46
8. Ubinadamu kihalisia huutazama msalaba kama hukumu ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu na huendelea kuamini uongo wa Shetani wa haki bila huruma. Isa 53:3,4
9. Visa vyote vya hukumu katika Bibilia ni ufunuo wa msalaba kwa sababu Kristo aliteseka katika mateso yote ya wanadamu. Isa 63:9. Jinsi tunavyohukumu visa hivyo ndivyo tutakavyohukumiwa. Matt 7:2

## Ibada ya Sanamu ya Ndama wa Dhahabu na Adhabu yake

Wacha sasa tutumie kanuni hizi katika kisa kimoja cha Agano la Kale.

> Kut 32:26-28 ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia (27) Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. (28) Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu.

Sasa zingatia maoni ya Roho ya Unabii

Musa aliagiza wale ambao walikuwa huru kwa dhambi hii kuu ya ibada ya sanamu, waje wasimame upande wa mkono wake wa kuume; pia, wale ambao walikuwa wamejiunga na waasi katika kuabudu sanamu, lakini walikuwa wametubu dhambi yao katika kuondoka kwa haraka kutoka kwa Mungu, wasimame kwa mkono wake wa kushoto. **Kulikuwa na kundi kubwa kabisa, sanasana la umati uliochanganyikana, ambao ulichochea kutengenezwa kwa ndamu, ambao walikuwa mkaidi katika uasi wao, na halingesimama na Musa**, kwa mkono wake wa kulia au wa kushoto. Kisha Musa aliamuru waliokuwa upande wake wa kulia wachukue panga, na waende wawaangamize waasi, ambao walitamani kurudi Misri. **Hakuna ambaye angetekeleza hukumu ya Mungu kwa waovu ni wale tu ambao hawakuwa wameshiriki katika ibada ya sanamu**. Aliwaamuru wasiache ndugu, wapenzi, wala jirani. **Wale ambao walihusika katika kazi hii ya mauaji, ijapokuwa chungu, sasa walikuwa watambue kwamba walikuwa wakitekeleza juu ya ndugu zao adhabu makini kutoka kwa Mungu. Kinyume na hisia zao wenyewe, Mungu angetawaza mibaraka yake juu yao**. Kwa kufanya kitendo hiki, walionyesha hisia zao za kweli sawia na [252] hatia kuu ya ibada ya sanamu, na walijiweka wakfu kikamilifu zaidi kwa ibada takatifu ya Mungu pekee wa kweli. 1SP 251, 252

Generali wa kweli kisha anachukua nafasi yake ya Mungu. Amekuja moja kwa moja kutoka kwa uwepo wa Bwana, ambapo alimsihi ageuze ghadhabu yake kutoka kwa watu wake waliopotea. Sasa ana kazi nyingine ya kufanya, kama mhudumu wa Mungu, kutetea heshima yake kwa watu, na kuwafanya kuona kuwa dhambi ni dhambi, na haki ni haki. Anakazi ya kufanya kukabiliana na athari ya kutisha ya Haruni "ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu. Musa akasema, Jiwekeni wakfu kwa Bwana leo, naam, kila mtu juu ya mwanawe na juu ya ndugu yake; ili awape baraka leo."

Hapa Musa anaelezea kujiweka wakfu kwa kweli kama utiifu kwa Mungu, kusimama katika uthibitisho wa nuru na kuonyesha utayari wa kutekeleza kusudi la Mungu katika majukumu ambayao sio yakupendeza zaidi, kuonyesha kwamba madai ya Mungu yako juu zaidi ya madai ya marafiki

> au maisha ya jamaa wa karibu. Wana wa Lawi walijiweka wakfu kwa Mungu kutekeleza haki dhidi ya ukaidi na dhambi. 3T 300,301

Kufupisha baadhi ya hoja muhimu

1. Watu walipewa toba kwa dhambi zao.
2. Umati mkubwa ulikataa kusimama na Musa. Hawakutubu na kukubali msamaha.
3. Musa aliamuru wale ambao hawakuwa wamehusika katika ibada ya sanamu kuchukua upanga wao na kuwaangamiza waasi bila kuzingatia hisia.
4. Hii ilikuwa adhabu kamili kutoka kwa Mungu.
5. Ilikuwa kazi ya uchungu ambayo kama ingetekelezwa ingewaletea baraka.
6. Ilielezea utakaso halisi na utiifu kwa Mungu.

Mwitikio asilia kwa kisa hiki ni kuhitimisha kwamba watu hawa walipigwa na Mungu na kuteswa. Ni asilia pia kuhitimishwa kwamba watu hawa walistahili kufa kwa sababu hawakuabudu miungu ya uongo tu bali pia walikataa kutubu kwa usumbufu. Kiasilia haki hutuambia kwamba Mungu aliwaua ili kuhifadhi taifa kwa sababu hawangetii kwa hali yoyote ile.

Inaonekana kuwa kisa wazi na kilichofungwa. Ni katika hatua hii itakuwa asilia kuhitimisha kwamba Mungu alisimama kama mtendaji kwa wadhambi hawa wakuu na hata kama haikuwa ya kupendeza, lazima ingetekelezwa. Ilikuwa bora kwamba hawa 3000 wafe badala ya taifa lote kuangamia. John 11:50.

## Unasoma Jinsi Gani?

Kwa wale ambao wanahubiri ujumbe wa Malaika wa Tatu tunaagizwa kufuata kanuni ya Miller za kufasiri Bibilia.

> Wale ambao wamehusishwa katika kuhubiri ujumbe wa Malaika wa tatu wanachunguza Maandiko kwa mpango sawia na ule ambao Baba Miller alikumbatia. Katika kitabu kidogo kiitwacho “Views of the Prophecies and Prophetic Chronology,” Baba Miller anatupa kanuni zifuatazo rahisi lakini zenye maarifa na muhimu kwa uchambuzi wa Bibilia na tafsiri:--

"1. Kila neno lazima liwe na gololi sahihi kuhusiana na mada ambayo imewasilishwa katika Bibilia; 2. Andiko lote ni muhimu; na linaweza fahamika kwa kuyaweka katika matumizi kwa uangalifu na kuyachunguza; 3. Hakuna chochote ambacho kimedhihirishwa katika Andiko kinaweza fichika au kitafichika kwa wale ambao wanaomba kwa imani, bila kusita; 4. **Kuelewa mafundisho, weka maandiko yote kuhusiana na mada unayotaka kujua pamoja, kisha wacha kila neno liwe na athari yake sahihi**; na kama unaweza unda nadharia yako bila ukinzani, hauwezi kuwa umekosea; 5. Andiko lazima lijifafanue lenyewe, kwa vile ni kanuni kivyake. Nikimtegemea mwalimu kunifafanulia, na atakisia maana yake, au atake iwe kwa upendeleo wa imani ya dhehebu lake, au kuonekana mwenye hekima, basi kukisia kwake, kutaka, imani, au hakima ni kanuni yangu, na sio Bibilia."

Zilizo hapo juu ni sehemu ya kanuni hizi; na katika somo letu la Bibilia sote tutafanya vyema kushika kanuni ambazo zimewekwa. RH, Novemba 25, 1884

## Kupima Kwa Uzima na Mauti ya Kristo

Hatufuati kanuni za Miller za kutafsiri kama tunafanya hitimisho yetu kabla ya kuleta sehemu zote pamoja. Vipande viwili vikubwa ambavyo lazima vihusishwe ni uzima na kifo cha Yesu. Maisha ya Kristo yanatwambia nini kuhusu hukumu ya Mungu?

Ebr 7:26 Kwa kuwa ilitupasa tuwe na Kuhani Mkuu wa namna hii, yaani, **aliye mtakatifu, asiye na lawama, asiye na dosari**, aliyetengwa na wenye dhambi na kuinuliwa juu ya mbingu;

Isa 53:9 Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; **Ingawa hakutenda jeuri**, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

"Herode na watawala waovo walimuua Mwenye Haki, **Lakini Kristo hakuua yeyote**, na tunaweza husisha roho wa kutesa—kwa sababu watu wanataka uhuru wa dhamiri—kwa asili yake—Shetani." Ms62-1886.64

Ebr 13:8 Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo na hata milele.

Yeshua kamwe hakuumiza yeyote, hakuwa mkatili na kamwe hakuua yeyote. Pia tunaweza kuwa na uhakika kwamba Kristo ni yule yule katika Andiko lote. Kazi ya Kristo ilikuwa gani katika kuja kwa ulimwengu huu:

> ...adui wa Mungu alipofusha mawazo ya wanadamu, wakamtazama Mungu kwa hofu; walimfikiria kuwa [11] mkatili na asiyesamehe. Shetani aliwafanya watu kumfahamu Mungu kama ambaye sifa yake kuu ni haki kali,--ambaye ni hakimu mkali, mkatili, mkopeshaji mkali. Alimpa Muumbaji taswira ya kiumbe ambaye anatazama kwa jicho la wivu ili kupambanua dosari na kasoro ya wanadamu, ili kwamba aweke hukumu juu yao. Kivuli hiki cha giza kilikuwa kiondolewe kwa kuudhihirishia ulimwengu upendo wa Mungu usiokuwa na mwisho, ndiposa Yesu kuishi miongoni mwa wanadamu. **Mwana wa Mungu alitoka Mbinguni kumdhihirisha Baba**. "Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha." John 1:18. Steps to Christ 10,11.

Katika ombi la kuvutia mno la Yesu tunamsikia akisema:

> John 17:6 Nimewajulisha Jina Lako wale ulionipa kutoka katika ulimwengu. Walikuwa Wako, ukanipa Mimi, nao wamelitii Neno Lako.

## Yesu anadhihirisha Jina/Tabia ya Baba

Jina la Mungu ni utukufu wake na utukufu wake ni tabia yake.

> Isa_42:8 Mimi ni Bwana; ndilo **jina** langu; na **utukufu** wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.

> Ebr 1:3 Mwana ni **mng'ao wa utukufu** wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni;

Kama tunavyoambiwa katika 'Steps to Christ', Yesu alikuja katika ulimwengu huu kudhihirisha tabia nzima ya Baba. Kama Yesu alivyomwambia Filipo:

> Yohana 14:9 Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, 'Tuonyeshe Baba?

Yesu alimwambia Filipo kwamba kutazama kwake kwa huduma ya Kristo kulimfanya kufuzu kujua hasa tabia ya Baba.

> Mungu hakuacha chochote ambacho angetekeleza kwetu bila kutekelezwa. **Alitoa mfano kamili wa tabia yake katika tabia ya Mwanawe;** na ni kazi ya wafuasi wa Kristo, wanapotazama uzuri usiolinganishwa wa

maisha yake na tabia, kukua kwa mfano wake. Wakimtazama Kristo na kupokea upendo wake, wataakisi sura ya Kristo RH, Feb. 15, 1898.

Tabia yote ya Mungu ilidhihirishwa katika Mwanawe. ST Dec 30, 1889

Upendo, heshima na ukamilifu unaodhihirishwa katika Injili ni ufunuo kwa mwanadamu wa tabia ya Mungu. Fadhili na wema na ukarimu ambao ulionekana katika tabia ya kristo zitarudiwa katika maisha ya wale ambao wanakubali fadhila za Injili. Kwa kusomaneno, tunafaa kumuona jinsi alivyo, na kufurahishwa na mtazamo wa ukamilifu wake mtakatifu, tunapaswa kukua katika mfano sawia. Tunahitaji kuelewa kwamba Injili kikamilifu hudhihirisha utukufu wa Bwana. Ni kioo ambacho hudhihirisha tabia ya Mungu kwa mioyo iliyoongoka. Mfano wa Mungu unadhihirishwa katika tabia kamilifu ya Mwanawe, ili tuweze kufahamu inamaanisha nini kuumbwa kwa mfano wa Mungu, na kwamba tunaweza kuwa tukiendelea kutazama tunaruhusu nafsi zetu kubadilishwa kutoka "utukufu hadi utukufu." ST Februari 24, 1909

Wale ambao wameshuhudia mibaraka ya Mungu wanafaa kuwa wenye shukurani zaidi miongoni mwa watu. Wanapaswa kunena kwa Mungu maneno ya shukurani kwa sababu **Kristo alikuja kwa mfano wa mwili wa dhambi, akiuvika uungu wake na ubinadamu, ili aweze kuleta kwa ulimwengu ukamilifu wa Mungu katika tabia yake mwenyewe. Alikuja kumwakilisha Baba, sio kama hakimu mkali, bali kama Baba mwenye upendo**. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Mungu ni Upendo. **Huu ulikuwa ukweli mkubwa ambao Kristo alikuja ulimwenguni kudhihirisha**. Shetani alikuwa amewasilisha tabia ya Mungu visivyo kwa ulimwengu, kwamba mwanadamu alikuwa mbali na Mungu; lakini **Kristo alikuja kuweka wazi kwa ulimwengu sifa za Baba, kuwakilisha sura ya moja kwa moja ya utu wake**. "Nami hufanya vile vile kama Baba alivyoniamuru." **Kiini cha kazi ya Kristo ulimwenguni kilikuwa kumdhihirisha Baba**. ST, April 11, 1895 par. 2

Kristo aliinua tabia ya Mungu, akimtukuza, na kumpa sifa, katika kazi yake yote duniani, —kuwaweka wanadamu sawa kupitia kufunuliwa kwa Mungu. Katika Kristo kulikuwa kumevikwa mbele ya wanadamu neema ya Baba na ukamilifu usio na kifani wa Baba. Katika ombi lake muda mfupi kabla ya kusulubishwa, alitangaza, "Nimewajulisha Jina Lako." "Nimekutukuza Wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye." Wakati kiini cha kazi yake kiliafikiwa, —ufunuo wa Mungu kwa ulimwengu,—Mwana wa Mungu alitangaza kwamba kazi yake

> imemalizika, na kwamba tabia ya Baba imejulikana kwa wanadamu. ST Januari 20, 1890, par. 9

Kazi ya duniani ya Kristo ilikuwa kumdhihirisha Baba na kuondoa uongo kwamba Mungu ni hakimu mkali na asiyesamehe. Tunaambiwa kwamba haki na huruma za Mungu inaonyeshwa katika kazi ya duniani ya Kristo. Yote ya tabia ya Baba yalidhihirishwa katika miaka hiyo 33. Ellen White anasema kwamba Yesu alitoa sura ya moja kwa moja ya tabia za Baba yake na hii ndio kazi alikuja kufanya. Katika ombi lake alimwambia Baba "nimemaliza kazi ulionituma kuifanya" na hiyo ilikuwa kudhihirisha jinsi Baba alivyo.

Yesu alitangaza jina au tabia ya Baba yake kikamilifu. Kwa hivyo visa vyote vya Bibilia lazima vihusishe ufahamu wa maisha ya Yesu duniani. Alikuwa asiyeweza kudhuru, sio mkatili na kamwe hakuua yeyote. Huo ndio ufunuo ambao tumepewa kumhusu Baba kupitia kwa Kristo.

Yesu alisema nini kuhusu matumizi ya upanga kama njia ya kujilinda?

> Matt 26:52,53 **Ndipo Yesu akamwambia, "Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga.** Je, unadhani siwezi kumwomba Baba yangu naye mara moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?

Yesu alimwambia Peter aweke kando upanga na kwamba amwamini Babake kumlinda kwa malaika zake.

# Yesu Kama Hakimu

Vipi kuhusu mifano ya hukumu katika maisha ya Yesu? Tunaona nini?

> Matt 23:31-38 Hivyo mnajishuhudia wenyewe kwamba ninyi ni wana wa wale waliowaua manabii. 32) **Haya basi, kijazeni kipimo cha dhambi ya baba zenu!** (33) **"Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka wenye sumu! Mtaiepukaje hukumu ya jehanam?** (34) Kwa sababu hii tazama nawapelekea manabii na wenye hekima na walimu. Baadhi yao mtawaua na kuwasulibisha, wengine mtawapiga mijeledi katika masinagogi yenu na wengine mtawafuatia kutoka mji mmoja hadi mji mwingine. (35) Hivyo ile damu ya wenye haki wote iliyomwagwa hapa duniani, tangu damu ya Abeli, ambaye alikuwa hana hatia, hadi damu ya Zekaria mwana wa Barakia, mliyemwua kati ya Patakatifu na madhabahu, itawajia juu yenu.

(36) Amin, nawaambieni, haya yote yatakuja juu ya kizazi hiki." Yesu Aililia Yerusalemu (37) "Ee Yerusalemu, mnaowaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka! (38) **Tazama nyumba yako imeachwa tupu na ukiwa.**

Viongozi wa taifa la Waebrania walikataa kumkubali Yeshua kama masihi. Kukataa huku kulipelekea kukataliwa kwa taifa lote kama wateule wake. Hili linamaanisha kwamba taifa lote la Israeli lilikuwa chini ya tishio kwa sababu ya viongozi hawa waasi. Sasa ingekuwa wakati wa kutumia upanga kama Yesu angetumia kwa sababu taifa lilihitaji kukombolewa! Haingekuwa bora kwa viongozi 3000 au kama hao wa Wayahudi kuuawa ili taifa nzima lisiangamie? Yesu alijibu vipi?

Matt 23:34 Kwa sababu hii tazama nawapelekea manabii na wenye hekima na walimu. Baadhi yao mtawaua na kuwasulibisha, wengine mtawapiga mijeledi katika masinagogi yenu na wengine mtawafuatia kutoka mji mmoja hadi mji mwingine:

Yesu angewatumia manabii na wenye hekima kuwasihi na hatimaye Yesu angewaacha kwa hila zao.

Matt 23:38 Tazama nyumba yako imeachwa tupu na ukiwa.

Wayahudi walighushi pingu zao wenyewe; walikuwa wamejijazia kikombe cha kisasi. Katika uharibifu wote ambao uliwapata kama taifa, na katika ole zote ambazo ziliwafuata katika kutawanyika kwao, walikuwa wakivuna tu mazoa ambayo mikono yao wenyewe ilikuwa imepanda. Anasema nabii: "Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako;" "maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako." Hosea 13:9; 14:1. Mateso yao mara nyingi yanawasilishwa kama sdhabu iliyowekwa juu yao kwa amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Ni katika hilo mdanganyaji mkuu anatafuta kuficha kazi yake mwenyewe. **Kwa kukataa kikaidi upendo tukufu na fadhili, Wayahudi walikuwa wamesababisha ulinzi wa Mungu kuondolewa kwao, na Shetani alikuwa ameruhusiwa kuwatawala kulingana na matakwa yake**. Ukatili wa kutisha uliotekelezwa katika [36] uharibifu wa Yerusalemu ni maonyesho ya nguvu za kisasi za Shetani juu ya wale ambao hufuata uongozi wake. GC 35.3

Mfano mwingine katika maisha ya Yesu ya Hukumu utakaso wake wa hekalu.

> Yohana 2:13-16 Ilipokaribia wakati wa Pasaka ya Wayahudi, Yesu alipanda kwenda Yerusalemu. (14) Huko hekaluni aliwakuta watu wakiuza ng'ombe, kondoo na njiwa. Nao wabadilisha fedha wakiwa wameketi kwenye meza zao. (15) Akatengeneza mjeledi kutokana na kamba, akawafukuza wote kutoka kwenye eneo la hekalu pamoja na kondoo na ng'ombe. Akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha na kuzimwaga fedha zao. (16) Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, "Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya nyumba ya Baba yangu kuwa mahali pa biashara?"

Mfano huu unaelezea jinsi Yesu hutekeleza hukumu. Wacha tufuate maoni katika Tumaini la Vizazi.

1. Kuhukumiwa kwa Dhambi

Kwa mtazamo wa kutafuta, kristo anachukua eneo la tukio lililoko mbele yake akisimama katika hatua za mahakama ya hekalu. Kwa jicho la utabiri anatazama mbeleni, na anaona sio tu miaka, bali karne na vizazi. Anaona jinsi makuhani na watawala watawageukia wasiojiweza katika haki zao, na kukataza kwamba injili ihubiriwe kwa masikini. Anaona jinsi upendo wa Mungu utafichwa kutoka kwa wenye dhambi, na watu watafanya neema yake kuwa biashara. **Anapotazama eneo la matukio, hasira, mamlaka, na nguvu zinaonyeshwa katika uso wake**. DA 157

2. Kwa wengi mawazo na nia husomwa na hatia husababisha kimya

Makini ya watu inavutwa kwake. Macho ya waliohusika katika biashara isio takatifu [158] yanaamrishwa kwa uso wake. Hawawezi ondoa kutazama kwao. **Wanahisi kwamba mtu huyu anasoma mawazo yao ya ndani, na anatambua nia yao iliyofichika**. Baadhi wanajaribu kuficha nyuso zao, kana kwamba matendo yao maovu yaliandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao, kusikaniwa na macho hayo ya utafiti.

**Mkanganyiko unanyamazishwa. Sauti ya biashara na majadiliano imesitishwa. Kimya kinakuwa kichungu.** Hisia ya hofu inakuwa na nguvu zaidi kwa umati. Ni kana kwamba walikuwa wameletwa mbele ya mahakama ya Mungu kujibu mashtaka ya matendo yao. Wakimtazama Kristo, wanaona uungu ukimulika ghafla kupitia kwa vazi la ubinadamu. Jemedali wa mbinguni anasimama kama Hakimu atakavyo simama katika siku ya mwisho,--sio sasa akizungukwa na utukufu ambao utamhudumia

wakati huo, bali kwa nguvu sawa za kusoma mioyo. Macho yake yanaufagia umati, nakuingiza kila mmoja. Umbo lake linaonekana kuinuka juu yao katika heshima ya kuamuru, na nuru takatifu inaangaza kipaji cha uso wake. DA 157, 158

3. Kuamriwa kuhusu tendo la dhambi.

Anazungumza, na sauti yake inayosikika vizuri—sauti ile ile ambayo Juu ya Mlima Sinai ilitangaza sheria ambaye makuhani na watawala wanaasi—inasikika katika mwangwi wa matao ya hekalu: "Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya nyumba ya Baba yangu kuwa mahali pa biashara." {DA 158.1}

4. Hukumu ya dhambi na nguvu iangamizayo inayotumiwa kwa vitu ambavyo havisongi hudhihirisha kutofurahishwa kwa Mungu.

Akikwea hatua polepole, na kuinua kamba za janga alijikusanya akiingia kwenye ua, anawaashiria kundi ambalo lina shauriana kuondoka kiungani mwa hekalu. Kwa jitihada na ukali ambao kamwe hajaonyesha awali, anageuza meza za wabadilishanaji wa sarafu. Sarafu zinaanguka, zikilia kwa sauti kali juu ya sakafu ya jiwe. Hakuna ambaye anathubutu kuuliza mamlaka yake. Hakuna ambaye anajaribu kukusanya fidia yake iliyopatikana kwa nia mbaya. **Yesu hawapigi kwa kiboko cha kamba, lakini mikononi mwake janga hilo rahisi linaonekana kutisha kama upanga wa moto**. Maafisa wa hekalu, makuhani wa kudadisi, mawakala na wauzaji wa ng'ombe, pamoja na kondoo na ndume zao, wanaharakisha kutoka mahali hapo, wakiwa na wazo moja la kuepuka hukumu ya uwepo wake. {DA 158.2}

5. Watu walikimbia badala ya kuomba msamaha.

Hofu inaufagia umati, ambao unahisi kulemewa na Uungu wake. Vilio vya kutisha vinatoweka kutoka kwa mammia ya midomo iliyotawanywa. Hata wanafunzi wanatetemeka. Wameshindwa na maneno na namna ya Yesu, kinyume kabisa na mwenendo wake. DA 158.3

Yesu hatendi ukatili wowote kwa watu. Kupitia kwa sheria wanahukumiwa na dhambi. Badala ya kumgeukia kwa kutubu walikimbia kwa sababu ya mtazamo wa mwanadamu wa haki bila huruma. Yesu alitaka kutakasa mioyo yao lakini walikataa kutubu na wakakimbia na kwa hivyo hekalu halisi likatakaswa. Dhambi iliwadanganya kwa sheria. Ingawa, hakuna yeyote

aliyeuawa na Yesu au kuvamiwa kikatili. Kutakaswa kwa hekalu kunaonyesha jinsi Baba huhukumu, kwa kuwa Yesu hudhihirisha Babake.

Mfano mwingine ni kulaani mtini.

> Matt 21:19-20 Akiuona mtini kando ya barabara, akaukaribia lakini hakupata tunda lo lote ila majani. Ndipo akauambia, "Wewe na usizae matunda tena kamwe!" Papo hapo ule mtini ukanyauka. (20) Wanafunzi wake walipoona jambo hili wakashangaa, wakamwuliza, "Imekuwaje mtini huu kunyauka ghafula?"

Mtini ulikuwa mfano wa hukumu.

> Tendo la Kristo katika kulaani mtini lilishangaza wanafunzi. Lilionekana kwao kama njia yake na kazi zake. Mara nyingi walikuwa wamemsikia akitangaza kwamba hakuja kuuhukumu ulimwengu, lakini kwamba ulimwengu kupitia kwake uokolewe. Walikumbuka maneno yake, "Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa." Luka 9:56. **Kazi zake za kupendeza zilifanywa kurejesha, sio kuangamiza kamwe. Wanafunzi walikuwa wamemjua tu kama Mrejeshi, Mponyaji. Tendo hili lilijisimamia pekee.** Kusudi lake lilikuwa lipi? Waliuliza. DA 582.2

> Mungu "hufurahia rehema." "Waambie, Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu." Mika 7:18; Ezekieli 33:11. Kwake kazi ya kuharibu na kukana ya hukumu ni "kazi ya ajabu." Isaya 28:21. Lakini ni katika fadhili na upendo kwamba huinua shungi kutoka maisha ya baadaye, na kudhihirisha kwa wanadamu matokeo ya mwendo wa dhambi. DA 582.3

> Kulaani kwa mtini ni mfano ulioigizwa. Mti huo tasa, ukitoa majani yake yenye uwezo wa kuzaa katika uso haswa wa Kristo, ulikuwa mfano wa taifa la Wayahudi. Mkombozi alitamani kuweka wazi kwa wanafunzi wake sababu na uhakika wa adhabu ya Israeli. Kwa kusudi hili aliwekeza kwa mti sifa za kimaadili, na kuufanya mwelezaji wa ukweli takatifu. DA 582.4

Mfano wa mtini ni muhimu kama mfano wa Hukumu. Yesu angeweza kuwaambia wanafunzi wake wakate mtini kwa shoka na upanga. Angeweza kuvunja matawi yake yote na kuuchoma kwa moto. Angeweza kufungua ardhi na kuumeza. Lakini aliuzungumzia tu na maji ambayo yalikuwa kwenye mti yakatoweka na kuufanya mti kunyauka. Maji ni ishara ya Roho na maji yaliondolewa kwenye mti kutuonyesha jinsi Roho wa Mungu huondolewa

kwa mdhambi. Katika mifano hii miwili ya utakaso wa hekalu na kulaaniwa kwa mtini tumeonyesha hukumu ya Mungu katika Mwanawe. Zingatia kwa makini kwamba Roho ya Unabii inasema tendo hili lilisimama lenyewe katika kazi ya uharibifu. Kwa hivyo mfano huu unakuonyesha jinsi Mungu huangamiza; huondoa Roho wake.

Wacha turejee kwa kisa cha Ndama wa Dhahabu na sasa tuangazie hoja zaidi. Swali madhubuti la kuuliza ni kama Walawi walijazwa na Roho wa Mungu walipowaua watu 3000. Walawi walikuwa katika Agano Jipya au Agano la Kale? Waisraeli wote walikuwa wamesema nini wiki chache awali?

> Kut 24:7 Kisha akakitwaa kitabu cha agano akakisoma masikioni mwa watu; wakasema, Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii.

Mungu alipowapa Israeli Agano Jipya Misri jibu la jumla lilikuwa lipi?

> Kut 6:8,9 Nami nitawaleta hata nchi ile ambayo naliinua mkono wangu, niwape Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo; nitawapa iwe urithi wenu; Mimi ni YEHOVA. Musa akawaambia wana wa Israeli maneno haya; lakini hawakumsikiliza Musa kwa ajili ya uchungu wa moyo, na kwa ajili ya utumwa mgumu.

Hakuna hata mmoja wa Waisraeli aliamini ahadi za Mungu. Hakuna rekodi ya kuashiria kwamba Walawi walikuwa kando na Israeli katika manuguniko na malalamishi. Hakuna rekodi yakuonyesha kwamba walikuwa wenye haki. Wote walikuwa katika Agano la Kale ambalo ni huduma ya mauti. Kwa hivyo Walawi walikuwa wanatenda kazi katika muktadha huo.

Swali lingine muhimu ambalo tunahitaji kuuliza ni mbona Israeli waliagizwa kutumia upanga? Yesu alimwambia Petro kuweka upanga wake kando. Mbona Yesu awaamuru Walawi kuchukua panga zao na kuwaua ndugu zao? Ni wapi tunapata upanga halisi ukitajwa mara ya kwanza katika Maandiko?

> Mwanz 27:40 Kwa upanga wako wewe utaishi, nawe utamtumikia nduguyo; Na itakuwa utakapoponyoka, Utalivunja kongwa lake katika shingo yako.

Isaka alimwambia Esau kwamba ataishi kwa upanga. Esau kamwe hakukubali Agano Jipya. Aliishi maisha yake yote katika Agano la Kale. Agano la Kale ni maisha ya kuishi kwa Upanga.

Kwa hivyo mbona Yesu akawaamuru Walawi kuwaua waabuduo sanamu? Tena tunakuja kwa maneno ya Kristo:

> Matt 7:2 Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea.

Kazi ya Sheria katika hukumu ya mauti ni kufanya dhambi iwe kubwa. Hili linamaanisha kwamba chochote ambacho mwanadamu anafikiria, Sheria itakuza wazo hilo na kulileta kwenye nuru. Zingatia tena kile ambacho Maandiko yanatwambia kuhusiana na suala hili:

> Eze 20:25 Tena naliwapa amri zisizokuwa njema, na hukumu ambazo hawakuweza kuishi kwazo;

Ni jinsi gani Baba yetu aliye mbinguni ambaye ni mwema anatupa chochote ambacho sio kizuri? Jibu ni kwamba huturuhusu kuhukumiwa na hukumu yetu wenyewe. Watu wa Mungu wanapopotoka kutoka kwa amri zake, mfumo wa haki usiokuwa na huruma wa Shetani unaruhusiwa kutawala. Mfumo wa haki sio mzuri lakini Mungu huuruhusu kuja ili kwamba dhambi za wanadamu ziadhibiwe kwa dhambi zao wenyewe.

> Bwana alisema kuhusu wana wa Israeli, "kwa sababu hawakuzitekeleza hukumu zangu, bali walizikataa amri zangu, nao walizitia unajisi sabato zangu, na macho yao yaliandama vinyago vya baba zao. Tena naliwapa amri zisizokuwa njema, na hukumu ambazo hawakuweza kuishi kwazo." **Kwa sababu ya kuendelea kwa uasi, Bwana aliweka adhabu kwa uasi wa sheria zake, ambazo hazikuwa nzuri kwa muasi**, au ambapo hangeishi katika uasi wake. 1SP 265.2

Katika kitabu *"God's of Egypt as Lightning from Heaven"* tunagundua kwamba amri ya kuwapiga watu kwa mawe hadi kifo ilikuwa tabia ya Wamisri (Kut 8:26) ambayo Waisraeli walipokea (Kut 17:4) na kisha ilijumuishwa katika Torah. (Law 20:27) mbona? Ni kwa sababu walihukumiwa walivyohukumu. Watu wanapokataa kuja katika Agano Jipya na kuhukumiwa kwa rehema wanasalia katika Agano la Kale na kuhukumiwa kwa hukumu zao wenyewe. Mbona basi inawasilishwa kama Mungu akiamuru? Sheria huingia ili dhambi ipate kuwa kubwa. Watu katika hali yao ya mwili wanaposikia Neno la Mungu wanaona uso wao wenyewe katika Sheria.

Yakobo 1:22,23 Basi iweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu. Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo:

Mtu aliye katika Agano la Kale hujidanganya kama dhambi kwa Sheria hutudanganya na kutuua. Mbona Mungu anaruhusu hili? Huwa anaacha mawazo yetu wenyewe kutuhukumu na kisha anatoa rehema kwetu kwa kutukaribisha katika Agano Jipya. Huduma ya Mauti iliyoandikwa kwenye jiwe hunena hukumu na kifo kwetu. Katika pahali hapa tukimgeukia Mungu tukiamini atatusaidia, kisha tunaweza ingia katika Agano Jipya. Tusipoamini atatusaidia basi tufe kulingana na hukumu yetu wenyewe.

## Abrahamu Anaagizwa Kumuua Mwanawe

Kuonyesha kwamba mawazo yalikuja ya kumtoa kafara Isaka.

Mwan 22:1-2 Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, *Mimi hapa*. (2) Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia.

Mbona Abrahamu alijaribiwa juu ya suala hili?

Mungu alikuwa amemuita Abrahamu kuwa baba wa imani, na maisha yake yalikuwa yawe mfano kwa vizazi vifuatavyo. Lakini imani yake haikuwa kamilifu. Alikuwa ameonyesha kutomwamini Mungu katika kuficha ukweli kwamba Sarah alikuwa mke wake, na tena katika ndoa yake na Haggai. Ili aweze kufikia kiwango gezi cha juu, Mungu alimweka wazi kwa jaribio lingine, karibu ambalo mtu daima aliitiwa kuvumilia. PP 147

**Kafara ambayo ilihatajika kwa Abrahamu** haikuwa pekee kwa uzuri wake, wala kwa manufaa kamili ya vizazi vijavyo; bali **kwa mafundisho ya viumbe wa mbinguni wenye maarifa wasio na dhambi na ulimwengu mwingine**. Uwanja wa mgogoro kati ya Kristo na Shetani ambapo mpango wa wokovu ulitendwa-ni kitabu cha mafunzo kwa ulimwengu. **Kwa sababu Abrahamu alikuwa ameonyesha ukosefu wa imani katika ahadi za Mungu, Shetani alikuwa amemshtaki mbele za malaika na mbele za Mungu kuwa alikuwa ameshindwa kufuata masharti ya agano, na kwa**

> **hivyo hakustahhili mibaraka yake**. Mungu alitaka kuthibitisha uaminifu wa mtumishi wake mbele ya mbingu yote, kuonyesha kwamba hakuna kitu kingine kuliko utiifu kamili kinaweza kubaliwa, na kufunua kikamilifu zaidi mbele zao mpango wa wokovu. PP 154

Abrahamu bado alikuwa na masalio ya kutokuamini moyoni mwake ambayo yalihitaji kuondolewa. Inawezekana kwamba Abrahamu alikuwa na hofu kwamba Mungu anaweza mwagiza amtoe mwanawe? Abrahamu alikuwa na ujuzi wa kafara ya mwanadamu?

> "Kisha Mkanaani alikuwa kwenye nchi." Abrahamu alikuwa amefikia lengo la matumaini yake kupata inchi ilimilikiwa na kabila la kigeni na kutawaliwa na ibada ya sanamu. **Katika vichaka kuliwekwa madhabahu ya miungu ya uongo, na kafara ya wanadamu ilitolewa juu ya milima ya majirani.** Aliposhikilia ahadi takatifu, haikuwa bila yenye kutazamia shida ambayo iliinua hema yake. PP 128

Pengine alihofu kwamba jambo lingetendeka kwa mwanawe. Kwa hali yoyote ile hofu kwamba jambo lingetendeka kwa Isaka ilikuwa hofu kwamba Mungu hangetimiza ahadi yake kwake. Lilikuwa jambo sawa na jinsi Ayubu alivyohisi?

> Ayubu 3:25 Maana jambo hilo nichalo hunipata, Nalo linitialo hofu hunijilia.

Ukweli kwamba Abrahamu alihofu kumwambia mke wake kuhusiana na agizo hilo ambalo lilipendekeza kwamba hakuwa na uhakika kuwa angemrejesha mwanawe. Katika safari ya siku chache kwelekea mahali pa kutolea kafara Abrahamu alipigana na mashaka yake na kisha hatimaye akajinyenyekesha na kumwamini Mungu kikamilifu.

Kumbuka kwamba kazi ya agano la kale ni kutuonyesha kwa kioo hali yetu ya dhambi. Kama vile kila kitu cha maisha ya usoni ya Abrahamu yalitegemea uzima wa Isaka, Abrahamu angekabiliana na hofu ya maisha ya usoni ya mwanawe kama angemuamini Mungu. Kama Abrahamu angemwamini Mungu basi hangekabiliana na jaribio hili. Sheria haiwezi akisi kile ambacho hakipo.

Tunaona jaribio sawa katika kisa cha Sulemani na wanawake wawili:

> 1 Wafalme 3:25-26 Mfalme akasema, Mkate mtoto aliye hai vipande viwili, kampe huyu nusu, na huyu nusu. (26) Ndipo mwanamke yule, ambaye mtoto aliye hai ni wake, akamwambia mfalme kwa maana moyoni mwake alimwonea mtoto wake huruma, akasema, Ee bwana wangu, mpe huyu mtoto aliye hai, wala usimwue kamwe. Lakini yule mwingine akasema, Asiwe wangu wala wako; na akatwe.

Agizo la kutumia upanga hudhihirisha kilichoko moyoni. Kama vile Sulemani aliamuru mtoto auawe kwa upanga ili aweze kudhihirisha kilichoko moyoni mwa akina mama hao wawili, ndivyo Mungu alivyomwamuru Abrahamu kumuua mwanawe ili kudhihirisha kilichokuwa moyoni mwake.

## Kuadhibu Dhambi kwa Dhambi

Kwa kiwango kingine, hukumu hii ilitoka kwa Mungu kulingana na hukumu yake mwenyewe. Ibrahimu alikuwa amechukua upanga kumlinda mpwa wake Loti na alikuwa ameishi kwa upanga ambao sasa alikuwa ameitiwa kuufia katika kumtoa kafara mwanawe. Kwa hivyo agizo hili la Mungu halikuja bila muktadha wake. Zingatia kile ambacho Ellen White anasema:

> Shetani alikuwa tayari kupendekeza kwamba lazima amedanganywa, kwa sababu sheria takatifu inaamuru, "Usiue," na Mungu hawezi hitaji kile ambacho amekataa. PP 148

> Kama ahadi hii ingetimizwa kupitia kwa Isaka, basi angeuawa aje? Abrahamu alikuwa amejaribiwa kuamini kwamba lazima alikuwa amedanganywa. Katika shuku yake na uchungu aliinama chini na akaomba, jinsi ambayo hakuwa ameomba awali, kwa udhibitisho wa amri kama lazima afanye jambo hili la kutisha. Akakumbuka kwamba malaika alitumwa kumuonyesha lengo la kuangamiza Sodoma, na yule ambaye alimfunulia ahadi ya mwana huyu huyu Isaka, na akaenda mahali ambapo alikuwa amekutana na mjumbe kutoka mbinguni mara kadhaa, akitarajia kukutana naye tena, na kupokea maelekezo zaidi; lakini hakuna ambaye alikuja kwa msaada wake. Giza ilionekana kumfunika; lakini amri ya Mungu ilisikiika masikioni mwake, "Mchukue mwanao sasa, mwanao wa pekee Isaka, ambaye unampenda." Amri hiyo lazima angeitii, na hakudhubutu kukuwia. Siku ilikuwa ikikaribia, na lazima awe safarini. PP 148.3

Hii ni hoja madhubuti ya kuzingatia. Mungu alipomjaribu Abrahamu kwa kumwagiza amuue mwanawe, Mungu alimwagiza kufanya kitu kiholela? La, inahusiana moja kwa moja na masuala ambapo anaogopa na ambapo hamwamini Mungu. Ili kumleta Abrahamu kikamilifu katika Agano Jipya lazima akutane naye katika la Kale ili kukabiliana na dhambi yake. hili linatatua mgogoro unaoonekana katika maneno haya:

> Shetani alikuwa tayari kupendekeza kwamba lazima adanganywe, kwa kuwa sheria takatifu inaagiza, "Usiue," na Mungu hangehitaji kile ambacho alikuwa amekataa wakati mmoja. PP 148

Mungu anawezaje amuru jambo ambalo wakati mmoja alikuwa amekataa? Sheria ni kiongozi wetu kutuleta kwa Kristo. Gal 3:24. Sheria huingia ili kosa liwe kubwa sana, Rum 5:20. Mungu hututia katika hukumu ambazo sio nzuri kulingana na mawazo yetu katika Agano la Kale ili kutuleta kwa hukumu ambazo ni nzuri katika Agano Jipya.

Hoja nyingine ya kuzingatia ni kwamba mashaka na hofu yetu hutusababisha kusoma visivyo maneno ya Mungu. Tambua hoja zifuatazo:

> Abrahamu alikuwa mwanadamu; shauku yake na mshikamano ulikuwa kama wetu; lakini hakuacha kuuliza jinsi ahadi itatimizwa kama Isaka angeuawa. Hakukaa kusemezana na moyo wake wenye maumivu. Mungu ni wa kweli na haki katika matakwa yake yote, na **na alitii agizo hadi mwisho**. {PP 153.3}

Kama Abrahamu alitii agizo hadi mwisho, basi Mungu alihitaji tu Abrahamu amtoe mwanawe wala sio kumuua. Abrahamu hakumuua mwanawe lakini roho ya unabii inasema alitimiza agizo hadi *mwisho*. Tofauti ni muhimu kwa sababu Mungu hakumuua mwanawe bali alimtoa. Hoja hii inadhibitishwa katika Yeremia.

> Yer 7:31 Nao wamepajenga mahali palipoinuka pa Tofethi, palipo katika bonde la mwana wa Hinomu, ili kuwateketeza wana wao na binti zao motoni; jambo ambalo mimi sikuliagiza, wala halikuingia moyoni mwangu.

Haikuingia moyoni mwa Mungu kuwatoa watoto kama kafara ya kuteketezwa kwenye madhabahu.

Tunaona kisa sambamba na hiki ni cha mwanamke wa kanani. Yesu alisema Si haki kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa. Matt 15:26. Alidhani kwamba alimuita mbwa lakini Yesu alikuwa anapima kiwango cha ubaguzi wa kikabila ndani yake na wanafunzi wake. Pengine alijibu kile ambacho kilisema alikuwa mwana wa Mungu lakini alielewa kwamba alikuwa mbwa lakini hata hivyo aliamini na kupokea hitaji lake. Katika kitabu cha Yohana tunaona mifano mingi ya watu wakipotosha maneno ya Yesu. Na Nikodemu, mwanamke kisimani na kuwalisha watu 5000 na mahali kwingine watu hawakumuelewa Yesu vilivyo na kufanya maneno yake kuonekana yasiyowezekana. Hii ni tabia ya wanadamu ambayo sheria huiweka wazi inapoingia.

Tutakapoelewa kanuni hii ya ukuzaji wa dhambi tunaweza thamini vyema kile kinachotendeka katika kisa cha kuwaua watu 3000 wenye ndama wa dhahabu. Wacha tuangalie kisa cha Eliya ili kuonyesha zaidi jinsi maagizo ya Mungu yanapotoshwa na wakati huo huo yanatimiliza matakwa yake.

## Eliya na Matumizi ya Upanga

Mchakato wa matumizi ya upanga pia yanaonekana katika kazi ya Eliya.

> 1 Wafalme 18:40 Eliya akawaambia, Wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja. Wakawakamata; na Eliya akawachukua mpaka kijito cha Kishoni, akawaua huko.
>
> Tena sauti ya Eliya inasikika katika maneno yenye kigugumizi akiwaamuru watu: "Wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja." Watu wako tayari kutii. Wanawakomesha manabii wa uongo [286] ambao walikuwa wamewadanganya, na kuwaletaka katika kijito cha Kishon, na hapo, kwa mikono yake mwenyewe, Eliya anawaua makuhani hawa wa kuabudu sanamu. 3T 285.1
>
> **Hukumu ya Mungu ikiisha tekelezwa juu ya makuhani wa uongo**, watu wakiisha ungama dhambi zao na kumthamini Mungu wa baba zao, laana ya kukausha ya Mungu sasa itaondolewa, na atafanya upya mibaraka yake kwa watu wake na kufanya upya inchi kwa umande na mvua. {3T 286.1}

Tunaambiwa kwamba amri ya Mungu ilitekelezwa kwa makuhani. Nini tena tunajifunza zaidi?

> **Mungu alitenda kupitia kwa Eliya alipowaangamiza manabii wa Baali** ambao waliwasha moto wa jehanamu katika moyo wa Yezebeli kulipiza damu ya makuhani wa Baali. Ushindi kama huo ulikuwa umepokelewa kwa Mungu wa Israeli, hilo lilichochea nguvu za giza, na aliamua, ndio anaapa kwa miungu yake kwamba lazima Eliya afe, lakini hazingatii kwamba kuna Mungu aliye juu yake, ambaye ataruhusu tu wakala wa Shetani kutenda maangamizi yake mwenyewe. 1888 488.1

Tambua inasema kwamba Mungu alitenda kupitia Eliya alipowaangamiza manabii wa Baali. Matendo ya Eliya yalionyesha tabia ya ufalme wa Mungu? Kujibu swali hili tunagundua jambo la kupendeza sana katika maisha ya Yohana Mbatizaji ambaye alikuja kwa uwezo na roho ya Eliya:

> Matt 11:2-3 Yohana Mbatizaji aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo Kristo alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi wake (3) ili wakamwulize, Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?

Mbona Yohana, mkuu katika manabii, alikuwa na mgogoro wa imani?

> Kama wanafunzi wa Mkombozi, Yohana Mbatizaji hakufahamu hali ya ufalme wa Kristo. Alitarajia Kristo achukue enzi ya Daudi; na kadri muda ulivyopita, na mkombozi hakudai chochote katika utawala wa kifalme, Yohana alishangazwa na kufadhaika. Alitangaza kwa watu kwamba ili njia inyooshwe kabla ya Bwana, unabii wa Isaya lazima utimizwe; Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa. Alikuwa ametazama pahali palipoinuka pa kiburi cha mwanadamu na uwezo pa kushushwa. Alikuwa amemwonyesha Masihi kama ambaye shabiki alikuwa mikononi mwake, na ambaye atasafisha kikamilifu sakafu yake, ambaye atakusanya ngano katika ghala lake, na kuchoma magugu kwa moto usiotzimia. Kama nabii Eliya, ambaye kwa roho na uwezo alikuwa amekuja kwa Israeli, alimtazamia Bwana kujidhihirisha kama Mungu anayejibu kwa moto. {DA 215.2}

Wala Yohana Mbatizaji, Wanafunzi wa Kristo au Eliya walielewa hali ya ufalme wa Kristo. Huu ni mshangao kwetu? Tambua kwamba tunaambiwa kuhusu malaika:

> Wenye hekima wa mbinguni walikuwa tayari kwa udhihirisho wa kutisha wa nguvu za mwenyezi. Kila hatua ilitazamwa kwa hamu kuu. Tendo la haki lilitarajiwa. **Malaika walimtazamia Mungu kuwaadhibu wenyeji wa**

> **dunia. Lakini Mungu alisema, nitamtuma Mwanangu**. Labda watamheshimu. "Mungu aliupenda ulimwengu akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele." **Neema ya ajabu! Kristo hakuja kuuhukumu ulimwengu, bali kuuokoa.** "Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu." Ms166-1898.27

Kwa hivyo hata malaika kabla ya Kristo kuja mara ya kwanza hawakuelewa kikamilifu tabia ya Mungu. Kama hili ni kweli kuhusu malaika basi tunaweza sema nini kuhusu wanadamu? Tukirejea kwa Eliya tunauliza swali, Eliya alianza lini kufahamu hali ya ufalme wa Mungu kwanza?

> Ukweli sawa ulifunuliwa kwa Yohana kama ulivyojitokeza kwa Eliya janwani, alipo "upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto, Mungu alinena na nabii kwa "sauti ndogo, ya utulivu." 1 Wafalme 19:11, 12. Kwa hivyo Yesu alikuwa atende kazi yake, sio kwa mgongano wa mikono na kugeuze tawala na falme, bali kwa kunena kwa mioyo ya wanadamu kwa maisha ya huruma na kujitolea nafsi. DA 217.2

Kwa hivyo hakufahamu hadi baada ya tukio la Mlima Kameli ndipo Eliya alianza kufahamu kwamba Mungu hakuwa katika Moto. Hata hivyo baada ya tukio hili Eliya alianguka tena kwa ufahamu wake wa kale?

Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana akapita.

> 2 Wafalme 1:10 Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake.

Tukio hili lilitendeka baada ya Eliya kukimbilia Mlima Sinai na akaonyeshwa kwamba Mungu hayuko kwenye moto. Yesu mwenyewe anatwambia kwamba Eliya hakuwa anawakilisha ufalme wa Mungu alipoagiza moto huu kushuka juu ya watu hao.

> Luka 9:54-56 Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: "Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?" (55) **Yesu akageuka na kuwakemea, akasema, Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo.** (56) kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa. Wakaondoka wakaenda mpaka kijiji kingine.

Mungu alitekeleza kupitia kwa Eliya maangamizi ya manabii wa Baali lakini aliadhibu dhambi ya manabii wa Baali kwa dhambi ya Eliya katika matumizi ya Upanga.

> Wakati wazazi au watawala wanapuuza jukumu la kuadhibu dhambi, Mungu mwenyewe atachukua jukumu hilo mikononi mwake. Uwezo wake ambao umezuiwa utakuwa katika kiwango ambacho kimetolewa kutoka kwa mashirika ya maovu, ili kwamba treni ya matukio itazuka ambayo itaadhibu dhambi kwa dhambi. PP 728.1

Ahabu hangeruhusu manabii wa Baali kufanikiwa, kwa hivyo Mungu aliruhusu mfululizo wa matukio kujifunua ambayo yangeadhibu dhambi kwa dhambi. Sasa kumbuka kwa sababu Yohana Mbatizaji alielewa ufalme wa Mungu visivyo alikuwa na mgogoro na imani. Jambo sawa lilitendeka kwa Eliya. Baada ya uzoefu wa Mlima Kameli alitarajia matengenezo kutendeka mara moja na hayakufanyika kwa sababu matendo ya Eliya hayakuwakilisha ufalme wa mbinguni.

> Ni nini Eliya aliona? Aliona kwa imani ahadi za Mungu? Alihesabu uaminifu wake katika kila jambo la ghafla lililopita? Hapana, kivuli cha giza cha shetani katika wakala wake Yezebeli alikuwa katika njia yake, akimtishia kwa kifo cha kikatili. Hakutazama mbinguni kupitia kwa kivuli hicho. Hofu ya kibinadamu ilishangaza na kupooza akili zake, na alikatizwa tamaa ajabu kwa ajili ya Israeli kiasi kwamba aliinuka na kuyakimbilia maisha yake, katika kukatishwa tamaa na uchungu zikikunja [489] hatua zake zisizo na uhakika, hakujua lolote. {1888 488.3}

> Muda mfupi kabla, katika nguvu za uwezo wa Mungu, alikuwa amejawa na jitihada na wingi wa mvuto wa Israeli waasi, wakikimbilia au upande wa gari la farasi la Ahabu. Alikuwa atetee utukufu wa Mungu. Alikuwa atie katika changamoto Waisraeli waasi wamtumikie Mungu kikamilifu au Baali kikamilifu. Lakini sana anaonekana dhaifu kama watu wengine. Hakuna neno halisi ambalo alikuwa amesikia kutoka kwa Bwana,

> likimwagiza achukue mwenendo ambao alikuwa amechukua, na hakukuwa kusudi la hatua zake. Akitatizwa na mashaka na ukosefu wa uhakika kama njia yake ilikuwa ya kutetea, aliiondoa njia hii na ile ya uzima wake, lakini Mungu hakumsahau Eliya. Alitenda kwa ajili ya mtumishi wake, aliuliza kumhusu, "Unafanya nini hapa Eliya?" 1888 489.1
>
> Historia ikisomwa kwa makini na kwa maombi itakuwa ya msaada kwa watu wa Mungu kati magumu. Kila mtu awe makini asitekeleze majukumu ambayo Mungu hahitaji kutoka kwake, na kujiweka kati ya Bwana na waliojaribiwa naye ili kusudi la Mungu lisitekelezwe katika uzoefu wa watu hawa. 1888 489.2

Shaka na kukanganyikiwa kwa Eliya kulikuja kwa sababu ya kuelewa ufalme wa Mungu visivyo. Kama Ellen White alivyosema:

> Ukweli sawa ulifunuliwa kwa Yohana kama ilivyojitokeza kwa Eliya jangwani, wakkati "upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; DA 217.2

Ni baada tu ya Mlima Kameli ndipo alianza kufahamu hali ya ufalme wa Mungu. Eliya alikuwa amechukua majukumu ambayo hakuwa amepewa na yalimsababishia kukata tamaa na kushindwa. Ila tunakumbuka kwamba "Mungu alitenda kupitia kwa Eliya alipowaangamiza manabii wa Baali." Ni jinsi gani Mungu alitenda kupitia Eliya katika hali hii? Zingatia kauli ifuatayo:

> Makuhani wa Baali wanashuhudia kwa bumbuazi ufunuo wa ajabu wa uwezo wa Yehova. Ila hata katika [154] fujo yao na katika uwepo wa utukufu wa uungu, wanakataa kutubu kwa matendo yao maovu. Bado wanasalia manabii wa Baali. Kwa hivyo walijionyesha kuivia maangamizi. Waliotubu katika Israeli wanaweza lindwa kutoka kwa ushawishi wa wale ambao wamewafundisha kuabudu Baali, **Eliya anaagizwa na Bwana kuwaangamiza walimu hawa wa uongo**. PK 153,154

Katika agizo la Mungu tunapata huduma ya mauti. Mungu alitangaza hukumu ya mauti kwa manabii wa Baali. Kama ambavyo tumejifunza, kusudi la hukumu hii ni kutia moyo wale ambao wamehukumiwa kutafuta rehema. Kukataa kutafuta rehema huja tu kutokana na ufahamu mbaya wa Mungu wa wale ambao wamehukumiwa na kwa hivyo hujiletea hukumu wenyewe

Mungu anapojiondoa kwao. Tunaona katika Kisa cha Musa kilichotendeka Mungu alipotangaza hukumu dhidi ya Israeli:

> Kut 32:10 Basi sasa niache, ili hasira zangu ziwake juu yao, niwaangamize, nami nitakufanya wewe uwe taifa kuu.

Agizo hili ni jaribio kwa Musa na Musa anajibu vipi?

> Kut 32:11 Musa akamsihi sana Bwana, Mungu wake, na kusema, Bwana, kwa nini hasira zako kuwaka juu ya watu wako uliowaleta kutoka nchi ya Misri kwa uweza mkuu, na kwa mkono wenye nguvu?

Musa anaomba kwa ajili ya watu Mungu anapoashilia kwamba atawaangamiza. Mbona Musa hakukubali tu agizo? Mbona alithubutu kukata rufaa dhidi ya hukumu ya Mungu? Kinachopendeza ni kwamba Mungu aliposema kwamba ataangamiza Israeli, Musa anaomba rehema lakini anapopewa hukumu ya kuangamiza baada ye anatekeleza hukumu hiyo.

> Kut 32:27 Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake.

Mungu alipotoa agizo la Kuwaua manabii wa Baali alikuwa anamkaribisha Eliya kuwaombea rehema watu hawa? Pia alikuwa anatafuta kutoa kwa Eliya hisia zake za ndani kwa watu hawa?

> 1Wafalme 19:10 Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na **kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu, waiondoe**.

Inawezekana kwamba Eliya alikuwa na hisia za ndani kuhusu ukweli kwamba rafiki zake waliuawa na manabii hawa wa Baali? Alikuwa na hofu na kukatishwa tamaa kwa sababu walijaribu kumuangamiza? Moto ulioshuka kutoka mbinguni ulionekana kuhalalisha kitendo cha kuwaua watu hawa kwa upanga? Wakati hukumu ya kifo ilitolewa na Mungu, Eliya alichukua jukumu juu yake ambalo hakuwa amepewa na je, alidhihirisha hisia zake za ndani hasi kwa manabii hawa ambazo zilifichika ndani yake? je, agizo la kuwaangamiza

manabii wa Baali lilikuza dhambi ndani ya Eliya ya nia ya kulipiza kisasi kwa kuwaua manabii wa Mungu na kuharibu taifa kwa ibada ya sanamu?

> Yakobo 5:17 **Eliya alikuwa mwanadamu kama sisi.** Akaomba kwa bidii kwamba mvua isinyeshe nayo haikunyesha juu ya nchi kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita.

Kama Eliya alikuwa huru kwa shauku kama tulivyo angejaribiwa kulipiza kisasi kwa kuuawa kwa watu wa Mungu na kwanza wale ambao walikuwa rafiki zake wazuri? Unaweza jaribiwa kulipiza kisasi rafiki yako wa karibu akiuawa, haswa kama haukufahamu hali ya ufalme wa Mungu?

Eliya aliagizwa kuwauwa manabii wa Baali kwa sababu hii ilikuwa huduma ya mauti na kutimiza mchakato wa Agano la Kale. Eliya hakuagizwa kuwaua manabii wa Baali *kwa upanga* bali Mungu *alitenda* kupitia kwa matendo haya kuwaadhibu Israeli na pia vilevile kukabiliana naye kwa hisia za ndani zake mwenyewe ambazo hazikuwa na uwiano na sheria ya Mungu.

Pili hakuna agizo katika Torah kutumia upanga kutekeleza haki kwa wenye hatia. Hukumu ya kifo kwa wale ambao wanaabudu mungu wa uongo ilikuwa kupigwa mawe hadi kufa.

> Kumb 13:6-10 Atakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mamaako, au mwana wako, au binti yako, au mke wa kifuani mwako, au rafiki yako aliye kama moyo wako, akikuambia, Twende tukaabudu miungu mingine usiyoijua wewe wala baba zako; (7) katika miungu ya mataifa yaliyo kando-kando yenu karibu nawe au mbali nawe, tokea ncha moja ya dunia hata ncha ya pili ya dunia; (8) usimkubalie wala usimsikize; wala jicho lako lisimwonee huruma, wala usimwache, wala usimfiche; (9) mwue kweli; mkono wako na uwe wa kwanza juu yake katika kumwua, na baadaye mikono ya watu wote. (10) Nawe mtupie mawe hata afe; kwa kuwa alitaka kukupotoa na Bwana, Mungu wako aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.

Kile ambacho Eliya alifanya kilikuwa kinyume na Torah kuhusiana na jinsi ya kukabiliana na ibada ya sanamu. Kile ambacho Eliya alizingatia kilikuwa utamaduni, utamaduni wa Israeli wa kutumia upanga. Katika mwanamke aliyeshikwa akizini tunaona jinsi mpaji wa sheria alikusudia hukumu yake ya kifo itekelezwe. Ilikuwa kumpa rehema kwa aliyetubu.

Hukumu ya Agano la kale iliadhibu dhambi ya manabii wa Baali kwa dhambi ya Israeli ya matumizi ya upanga na wakati uo huo ilimfanya Eliya kuelewa hisia zake za ndani. Vipi tena tunaweza elezea hofu ya Eliya ya ghafla machoni mwa Yezebeli? Kushindwa huku kwa upande wake kunadhihirisha kwamba Shetani alikuwa ameruhusiwa kumfikia kwa njia fulani? Inawezekanaje tena kusawazisha matumizi ya Eliya ya upanga na maneno ya Yesu?

> Matt 26:52 Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga.

Tabia ya Yesu inadhihirisha kwamba hawezi tumia upanga halisi na Petro alipoutumia, alimponya mtu ambaye alivamiwa na kumkemea Petro. Mahali ambapo Yesu alitaka Petro aweke upanga wake ni mbali na mikono yake. Alitaka Petro awe kama yeye ambaye kamwe hakutumia upanga halisi wakati wowote.

## Kasi ya Musa

Musa alikuwa na uzoefu sawa na Eliya? Tunakumbuka kwamba Musa hakufahamu hali ya Ufalme wa Mungu alipomuua Mmisri.

> Musa aliharakisha katika kumuua Mmisri. Alidhani watu wa Israeli walifahamu kwamba utoaji wa riziki ya kipekee ya Mungu ulikuwa umemuinua kuwakomboa. **Lakini Mungu hakubuni kukamilisha kazi yake kwa vita, kama Musa alivyodhani, bali kwa uwezo wake mkuu, ili utukufu upate kuhesabiwa kwake pekee.** Ingawa tendo hili la haraka lilibatilishwa na Mungu kuleta kusudi lake. ST Feb 19, 1880

Ukombozi wa Israeli haukuwa ukamilishwe kwa vita. Hakuna hata sehemu moja ya huduma hii kutoka Misri hadi Kanani ilikuwa itendwe kwa njia hii. Roho ya unabii inaita hili tendo la haraka. Musa alitenda kwa haraka alipomwambia Yoshua achukue upanga na apigane na Waameleki?

> Kut 17:8-9 Wakati huo Waamaleki wakatokea, wakapigana na Israeli huko Refidimu. (9) Musa akamwambia Yoshua, Tuchagulie watu, ukatoke upigane na Waamaleki; kesho nitasimama juu ya kilele kile, na ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu.

Kutoka 17:9 inapaswa kusomwa kwamba Musa alimwagiza Bwana kile ambacho atafanya lakini haisemi hivi. Sifa kuharakisha ilidhihirisha hapa

tena? Ni ukweli kwamba Musa aliwekwa katika nafasi ya kutisha. Wana wa Israeli hawakumwamini wala Mungu na walilalamika kuhusiana na kila kitu na hata wakataka kumpiga Musa kwa mawe. Lakini kwa kuchukua upanga wakati mmoja kuwalinda Israeli dhidi ya Waamaleki, upanga sasa ungerejea kwa Israeli na wengi wao wakafa kwa upanga.

Tunapokuja kwa kisa cha ndama wa dhahabu tunaona sifa ya kuwa na kasi tena?

> Musa alipoona ibada ya sanamu ya Israeli na hasira yake [301] aliamshwa na kusahau kwao kwa aibu kwa Mungu kiasi kwamba alitupa chini mawe mawili ya Amri na yakavunjika, Haruni alisimama kando yake kwa unyenyekevu, akibeba lawama ya Musa kwa uvumilivu wa kupongezwa. **Watu walivutiwa na roho ya Haruni ya upendo na walikasirishwa na kasi ya Musa.** Lakini Mungu haoni kama mwanadamu aonavyo. Hakulaumu shauku na hasira ya Musa dhidi ya uasi wa Israeli uliokithiri. 3T 300

Mungu aliujua moyo wa Musa hata ingawa alitenda kwa kasi. Mungu alitenda kupitia kwa Musa ili kuwaamsha Israeli kutoka kwa uovu wa dhambi zao. Musa alipochukua upanga kukabiliana na Waamaleki alikuwa akisimama katika dhambi za baba zake na kufanya kile mtu yeyote asilia anaweza fanya yaani kuilinda familia yake.

## Unabii wa Yakobo kuhusu Lawi

Matendo ya Musa hayakuwa kwake pekee. Kitambo sana kabla ya Musa kuzaliwa, maneno yafuatayo yalinenwa kuhusu kiongozi asilia wa kabila lake.

> Kut 49:5-7 Simeoni na Lawi ni ndugu; Panga zao ni **silaha za jeuri**. (6) Nafsi yangu, usiingie katika siri yao, Fahari yangu usiungane na kusanyiko lao, **Maana katika ghadhabu yao walimuua mtu, Na kwa ukaidi wao walikata mshipa wa ng'ombe;** (7) **Ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali, Na hasira yao, maana ilikuwa haina huruma. Nitawagawa katika Yakobo, Nitawatawanya katika Israeli.**

Tunapoangalia katika siku za usoni, Yakobo kwa kuongozwa na roho alitabiri kuhusu kabila la Lawi na vilevile la Simeoni. Ghadhabu ya Lawi ilikuwa laana na ni ghadhabu hii ndio Musa alikuwa apigane nayo katika uzoefu wake hadi mwisho wa maisha yake ya ulimwenguni. Tunaona ghadhabu hii

ikidhihirishwa kwa Phineasi ambaye aliwachoma mkuki wadhambi ambao walikuwa wanasababisha mapigo kushuka kwao. Walawi waliweka wazi chuki yao kwa ibada ya sanamu na matendo hasi ya ndugu zao.

Mbona basi Mungu akachagua kabila la Lawi kuwa la ukuhani? Tunahitaji kurejea kwa kisa cha Yusufu ili kuelewa hili.

> Mwanz 37:28 Wakapita wafanya biashara Wamidiani; basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini; nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri.
>
> Wazo la kuuzwa kama mtumwa lilikuwa la kutisha zaidi kwa Yusufu kuliko kuuawa. Alionyesha uchungu mwingi, na wito mwanzo kwa ndugu zake, kisha kwa mwingine, kwa huruma. Baadhi ya mioyo yao ilimhurumia, lakini kwa hofu ya kuzomewa na wengine, walinyamaza. Wote walidhani kwamba walikuwa wameenda mbali zaidi ya kuungama matendo yao; kwa sababu Yusufu anaweza waanika kwa baba yao, na atakasirishwa zaidi nao kwa yale waliomtendea Yusufu huyu aliyependwa sana. **Walikausha mioyo yao dhidi ya huzuni, na hawangesikiza maombi yake kwa sababu ya baba yake na kumuacha aende zake, bali wakamuuza kama mtumwa.** {1SP 129.2}

Nduguze Yusufu walifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya kilio cha moyoni cha huruma. Kwa kumuuza ndugu yao utumwani bila huruma, walipanda mbegu ambayo ingesababisha wanao kuuzwa utumwani na kutawaliwa bila huruma. Kama Andiko linavyosema:

> Yakobo 2:13 Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu.

Roho ya unabii inatwambia kwamba Simeoni na Lawi ndio waliokuwa na hatia zaidi kuhusiana na jinsi ndugu walivyomtendea Yusufu.

> Kisha alitabiri kuhusiana na **Simeoni na Lawi**, ambao walifanya uongo kwa Waishmaeli, na kisha, kwa namna ya kulipisha kisasi, kikatili, wakawaangamiza. **Bado ndio waliokuwa na hatia zaidi katika hatima ya Yusufu.** Simeoni na Lawi ni ndugu; Panga zao ni silaha za jeuri. 1SP 154, 155

Wakati ambao dada yao alipozwa na kijana Shekemu, witikio wao ulikuwa ujeuri wa uasi uliowekwa wazi kaktika mauaji ya Waishmaeli.

> Ujeuri wa usaliti wa Simeoni na Lawi haukuwa usio wa kuchochewa; ila katika kutenda kwaa kwa Waishamaeli walifanya dhambi chungu. Walikuwa wamemfichia Yakobo kwa makini kusudi lao, na tangazo la kulipisha kisasi kwao lilimjaza hofu. Kwa kuvunjwa moyo na udanganyifu na ukatili wa wanawe, alisema tu, "Mmenitaabisha, kunifanya ninuke vibaya kati ya watu wa nchi hii: . . . na mimi, kwa kuwa watu wangu ni haba, watanikusanyikia, na kunipiga, nami nitaangamizwa, mimi na nyumba yangu." Lakini huzuni na chuki ambayo alichukulia matendo yao inaonyeshwa na maneno ambayo, karibu miaka hamsini baadaye, alirejelea, alipokuwa akilala katika kitanda chake cha mauti Misri: "Simeoni na Lawi ni ndugu; Panga zao ni silaha za jeuri. Nafsi yangu, usiingie katika siri yao, Fahari yangu usiungane na kusanyiko lao. . . . Ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali, Na hasira yao, maana ilikuwa haina huruma." Genesis 49:5-7. {PP 204.3}

Huku Kuwa tayari kuua kwa uasi kungetembelea Israeli Mlima Sinai na mahali pengine kwa sababu unabii wa Yakobo ulikuwa wa siku za mbeleni.

> Yakobo alipozungumza na wanawe mara ya mwisho, Roho wa Mungu alikaa juu yake, na **akatamka unabii kuwahusu, ambao ulitokea mbali zaidi katika siku za mbeleni.** Akiwa katika mwongozo war oho, aliweka wazi kwao maisha yao ya awali, na historia yao ya siku za mbeleni, **akidhihirisha kusudi la Mungu kuhusiana nao.** 1SP 154

Mungu alifanya kupitia kwa ujeuri wa Lawi kuadhibu dhambi za Israeli. Tabia ya ukuhani ambayo Israeli walijua na kukusudia ilikuwa tu tabia ambayo ilipatikana katika kabila la Lawi na kwa hivyo ikawekwa juu ya Israeli.

Katika kisa cha kuwaua watu 3000, maovu ya baba juu ya watoto hadi kizazi cha tatu na cha nne sasa yalirejelewa. Mungu huamru tu kwa Sheria ambayo Walawi walifikiria jinsi inaweza kabiliwa. Bwana anajaribu uaminifu wa Walawi kwa sababu ya ukosefu wao wa uaminifu awali kwa kutokubali Agano Jipya. Mibaraka ambayo ilimjilia Abrahamu kwa kutii agizo la kumtoa mwanawe ilikuwa kwamba iliponya ukosefu wake wa imani kwa Mungu na hili lilibariki ulimwengu kwa kuonyesha mfano wa Msalaba.

Israeli walipofanya dhambi kwa ndamu wa dhahabu Sheria iliingia na kufanya dhambi kuwa kubwa. Dhambi zao za awali za kutumia upanga kama taifa sasa zilikuwa zikirejelewa juu yao kupitia kwa Agano la Kale. Mbaraka ambao ulikuja kwa Israeli ulikuwa kutambua jinsi dhambi ilikuwa mbaya kweli na kwa wakati huo kujifunza kuwa watiifu wakati ambao ni vigumu. Ingawa tena tunasisitiza kwamba hakuna wakati ambao yeyote katika Waisraeli hawa alikuwa katika Agano Jipya. Hakuna wakati walijazwa na Roho wa Yesu walipokuwa wakiwaua watu hawa kwa sababu hakuna ukatili katika Roho wa Kristo.

Bwana alikuwa akitoa msamaha kupitia kwa Musa alipowauliza ni nani aliyeupande wa Bwana. Watu hawa walipokataa kutubu, wangekabiliana na ufahamu wao wenyewe wa hukumu. Dhambi ya matumizi ya upanga ilifanywa kubwa kupitia kwa Sheria na Mungu aliadhibu dhambi kwa dhambi.

> Kut 20:5 Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao;

Israeli waliinamia sanamu na Mungu alirejelea uovu wao kwa uovu wa Walawi, uliotabiriwa na Yakobo Karne nyingi za awali, katika matumizi ya Upanga. Wangeishi kama Esau ili kudumu.

Wale ambao waliangamia wengi walikuwa ambao walikuwa wamejiunga na Israeli na waliitwa umati uliochanganyika.

> Musa alitoa wito kwa watu, "Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu." Wale ambao hawakuwa wamejiunga na uasi walikuwa wachukue nafasi zao upande wa kuume wa Musa; waliokuwa na hatia lakini wakatubu upande wa kushoto. Walitii amri. Ilipatikana kwamba kabila la Lawi hawakuhusika katika ibada ya sanamu. Kutoka kwa makabila mengine kulikuwa na number nyingi ambao, ingawa walikuwa wamefanya dhambi, sasa walionyesha kutubu kwao. **Lakini kundi kubwa, haswa la umati uliochanganyika ambao ulichochea kutengenezwa kwa ndama, kwa ukaidi waliendelea kwa uasi wao.** PP 324

Waishmaeli walikuwa wamefanya agano la kujiunganisha na familia ya Yakobo na kuruhusu wana wao wa kike na kiume kuoana.

> Kut 34:8-10 Hamori akasema nao, akinena, Roho ya Shekemu, mwanangu, inamtamani binti yenu, tafadhalini, mpeni amwoe. (9) Mkaoane na sisi, mtupe sisi binti zenu, nanyi mkatwae binti zetu. (10) Nanyi mtakaa nasi, na nchi hii itakuwa mbele yenu; kaeni, na kufanya biashara humo, mkapate mali humo.

Walawi kuua umati uliochanganyika katika Mlima Sinai ambao ulikuwa umejiungamanisha na Israeli ilikuwa ukuzaji wa mauaji ya Waishmaeliambao walikuwa wajiungamanisha na Israeli karne nyingi awali. Katika kudhihirisha dhambi za baba yao wa kwanza Lawi, walawi walikuwa na fursa ya kumtafuta Bwana kwa ukatili wa kuwaua watu kwa upanga. Walawi walipoenda kulala usiku huo na kuona nyuso zilizoteswa za watu waliokufa katika ndoto zao na kwa uwezekano wakaamuka kwa hofu ya mazingira ya mauti, walikuwa na wakati wa kugeuka kutoka kwa ukatili wao na kutafuta njia bora.

Katika kusimulia watu 3000 ambao waliangamia tunao uzoefu sambamba wa msalaba. Kristo alitaka kuwaokoa watu hawa 3000 lakini walikataa kutubu. Walikataa kufikia na kuamini kwamba Mungu anaweza wasamehe. Kama Kristo walikufa chini ya hukumu ya dhambi. Tofauti na Kristo hawakujiweka mikonono mwa Baba kwa sababu hawakumwamini.

## Kutolewa Kama Fidia

Na kwa hivyo tunaona msalaba katika kifo cha watu hawa kwa sababu tayari neema ilikuweko kwao lakini hawakuipokea. Kifo chao kiliwafanya Israeli kutetemeka kwa hatari na ukali wa dhambi na hili liliwafanya watu kunyenyekea na kuwakaribisha kwa Agano Jipya. Kama Misri ilivyotolewa kama fidia kwa Israeli (Isa 43:3) ndivyo 3000 walivyotolewa kuwagutusha Israeli kumgeukia Mungu na kutafuta msamaha. Jinsi Kristo alivyohisi hukumu ya dhambi kupitia kwa Sheria ndivyo wale ambao walikataa kuja kwa Musa na kuokolewa. Kwa huzuni kwa sababu hawakuukubali msalaba wa Kristo walikufa wao wenyewe.

Tukiona kwamba Mungu aliruhusu kifo cha Mwanawe kwa sababu ya dhambi basi tutaona kwamba Mungu aliruhusu kifo cha watu hawa 3000 Sinai. Tukiona kwamba dhambi ilimuua Kristo alipofanyika dhambi kwa ajili yetu na hili lilisababibisha sheria kuwasilishwa kama yenye kuhukumu bila tumaini,

basi tunaweza ona kwamba dhambi iliwaua watu hawa 3000 kule Sinai kwa sababu sawa. Nawasihi usione watu hawa walipigwa na Mungu na kuteswa bali kupokea hukumu kupitia Sheria kulingana na mtazamo wao wenyewe wa Mungu na Sheria.

Mchakato huu umeelezewa wazi na Yesu.

> Mat 25:24-30 Kisha yule mtumishi aliyepokea talanta moja akaja, akasema, 'Bwana, **nilijua kwamba wewe ni mtu mgumu, unayevuna mahali usipopanda na kukusanya mahali usipotawanya mbegu**. (25) Kwa hiyo niliogopa, nikaenda, nikaificha talanta yako ardhini. Tazama, hii hapa ile iliyo mali yako.' (26) "Bwana wake akajibu, 'Wewe mtumishi mwovu na mvivu! Ulijua kwamba ninavuna mahali nisipopanda na kukusanya mahali nisipotawanya mbegu. (27) Vema basi, ingekupasa kuweka fedha yangu kwa watoa riba, nirudipo, nichukue ile iliyo yangu na faida yake? (28) 'Basi mnyang'anyeni hiyo talanta mkampe yule mwenye talanta kumi.' (29) Kwa maana kila mtu mwenye kitu ataongezewa, naye atakuwa navyo tele. Lakini kwa mtu yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. (30) "Nanyi mtupeni huyo mtumishi asiyefaa nje, kwenye giza, mahali ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.

Giza la nje ndipo Yesu alikuwa msalabani. Ni hukumu ya dhambi bila tumaini la msamaha. Mtu aliyekuwa na talanta moja angesamehewa lakini aliamini Bwana wake alikuwa mtu mwenye moyo mgumu na kwa hivyo haingewezekani amsamehe.

Kupitia kwa kuunganisha visa vya Abrahamu, Musa, Eliya, na Yohana Mbatizaji katika mfumo huu, tabia ya Mungu inayodhihirishwa katika Kristo, tunaweza anza kuelewa kilichofanyika kwa agizo la kuwaua walioasi na kukataa toba na Ndama wa Dhahabu.

Huduma ya mauti ni tukufu. Inauwezo wa kuwatoa watu katika Agano la Kale kwa Agano Jipya, na wakati huo huo ikileta mauti na maangamizi kwa wale ambao hukataa kukubali hukumu yao, kwa njia ambayo ni kulingana na hukumu yao wenyewe. Hekima ya Baba yetu katika hili ni ya ajabu kwangu. Nataka kuletwa kikamilifu kwa Agano Jipya. Nashukuru kwa Agano la Kale ambalo hunitia hatiani kwa dhambi zangu na hunihukumu hadi kwa kifo. Ila kwa vile naona upendo wa Baba kama mwenye huruma daima na ninaamini kwamba Yesu ameshinda hukumu hiyo basi ninafurahia kuja katika Agano

Jipya kwa Kristo na kujua kwamba nimesamehewa kikamilifu na kupatiwa haki ya Kristo kama urithi wangu.

Kila siku ninapotiwa hatiani kwa dhambi, namshukuru Baba kwa Agano la Kale lenye uwezo wa kunionyesha hitaji langu kuu na kunifanya kuona kwamba nitakufa. Kisha ninafurahia kuelekezwa kwa Kristo ambapo ninapokea haki. Agano zote zinatenda kazi kwa wokovu wangu. Moja linaua utu wangu wa zamani na lingine linanileta kwa ufufuo wa Kristo kama Bwana wangu.

# Huduma ya Mauti

Mbona Yesu alimwambia Petro aweke kando upanga wake lakini anawaambia walawi kupitia kwa kambi na kuwaua wale ambao walikataa kutubu?

> Kut 32:26-28 ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia (27) Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. (28) **Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa**, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu.

Na unapata nini kwa maoni haya?

> Wale ambao walijihusisha katika kazi hii ya kuchinja, ingawa chungu, sasa walikuwa watambue walikuwa wakitenda juu ya ndugu zao na adhabu kamili kutoka kwa Mungu; na kwa utekelezaji wa kazi hii chungu, kinyume na hisia zao wenyewe, Mungu atahifadhi mibaraka juu yao. 1SP 252

Tunaweza leta aje uiano kwa vitu hivi?

> Ajabu ya msalaba huelezea maajabu mengine yote. Katika nuru ambayo hutiririka kutoka Kalvari sifa za Mungu ambazo zilikuwa zimetujaza na hofu na uoga zinaonekana kupendeza na kuvutia. Rehema, huruma, na upendo zinaonekana kuchanganyika na utukufu, haki na uwezo. Tunapotazama ukuu wa enzi yake, juu na kuinuka zaidi, tunaona tabia yake katika dhihirisho la neema yake, na kufahamu, kuliko awali, umuhimu wa jina hilo la kupendeza, « Baba Yetu." GC 652.1

Tuuchunguzapo msalaba tunaona kwamba kweli huduma ya mauti ni tukufu na inawakaribisha wale ambao wanaamini ahadi za Mungu katika Haki yake.